**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA UCHAGUZI NAM. 11 YA 1984**
**NA KUTUNGA SHERIA YA UCHAGUZI YA MWAKA 2017**
**NA MASUALA MENGINE YANAYOHUSIANA NAYO**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SURA YA KWANZA
### MASHARTI YA UTANGULIZI


1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Kusomwa.
3. Tafsiri.
4. Majukumu ya Tume.


### SURA YA PILI
### SEHEMU YA KWANZA
### DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA


5. Kuanzishwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.
6. Matumizi ya Daftari.
7. Ufungaji wa Daftari.
8. Maafisa Uandikishaji na Makarani Uandikishaji.
9. Majukumu ya Karani wa Uandikishaji.
10. Uwezo wa Karani wa Uandikishaji


### SEHEMU YA PILI
### UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA


11. Wakati na eneo la Uandikishaji.
12. Sifa za kuandikishwa.
13. Taratibu za Uandikishaji.

14. Sheha kuwa wakala wa uandikishaji kwa wadhifa wake.

15. Wakala wa Uandikishaji.

16. Watu wanaoruhusiwa katika kituo cha uandikishaji.

17. Kukataliwa kwa maombi ya kuandikishwa.

18. Uamuzi wa Tume juu ya Rufaa.

19. Kuweka Wazi Orodha za Waombaji.

20. Malalamiko dhidi ya orodha iliyowekwa wazi.

21. Pingamizi ya Muombaji.

22. Kuingizwa katika Daftari.

23. Kitambulisho cha Mpiga kura.

24. Kitambulisho kilichopotea au kuharibika.

**SEHEMU YA TATU**
**UKAGUZI WA DAFTARI**

25. Ukaguzi wa Daftari.

26. Malalamiko dhidi ya Daftari.

27. Pingamizi dhidi ya mtu aliye katika Daftari.

28. Uchunguzi na maamuzi ya Afisa Uandikishaji.

**SEHEMU YA NNE**
**UENDELEZAJI WA DAFTARI**

29. Uhamisho wa taarifa za Mpiga Kura.

30. Maombi ya kubadilisha taarifa za mpiga kura aliyeandikishwa.

31. Kumwondoa mpiga kura asiyekuwa na sifa.

32. Kuweka wazi orodha ya wapiga kura wanaohamisha taarifa na waliopoteza sifa.

33. Kubadili jina.

## SURA YA TATU
## SEHEMU YA KWANZA
## UCHAGUZI MKUU


34. Uchaguzi Mkuu.

35. Watu wenye haki ya kupiga kura.

36. Msimamizi, Msaidizi Msimamizi wa uchaguzi na watendaji wa vituo.

37. Maeneo ya kupigia kura.

38. Taarifa ya Uchaguzi.

39. Ubandikaji wa Daftari katika eneo la kupigia kura.

40. Uchaguzi mdogo.

41. Uchaguzi wa marudio.


## SEHEMU YA PILI
## UTEUZI WA WAGOMBEA


42. Siku ya uteuzi.

43. Sifa za Mgombea wa Urais.

44. Sifa za Kugombea Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi.

45. Sifa za Mgombea wa Udiwani.

46. Fomu ya Uteuzi.

47. Uchukuwaji na Urejeshaji wa Fomu za wagombea.

48. Wadhamini wa Mgombea.

49. Dhamana.

50. Uwekaji wazi wa fomu za uteuzi.

51. Pingamizi dhidi ya uhalali wa fomu ya uteuzi.

52. Rufaa dhidi ya Uamuzi wa uteuzi.

53. Uteuzi wa Viti maalum.

54. Utaratibu wa uteuzi.

55. Taarifa ya uteuzi.

56. Nafasi ya wazi ya viti maalum vya Wanawake.

57. Taarifa na shahada ya uteuzi.

58. Mgombea pekee wa Urais.

59. Mgombea pekee wa Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi au Udiwani.

60. Kujitoa kwa mgombea.

61. Kifo au kukosekana kwa mgombea.

**SEHEMU YA TATU**
**KAMPENI ZA UCHAGUZI**

62. Kampeni za Uchaguzi.

63. Mkutano wa hadhara.

64. Vifaa vya kampeni na ubandikaji wake.

65. Kanuni za Maadili.

66. Kampeni za Vyombo vya habari vya Umma.

**SEHEMU YA NNE**
**MATAYARISHO YA UPIGAJI KURA**

67. Maeneo na Vituo vya kupiga Kura.

68. Upangaji wa Vituo vya kupiga Kura.

69. Wajibu wa msimamizi wa kituo.

70. Uwezo wa msimamizi wa kituo.

71. Vifaa vya kupigia kura.

72. Karatasi ya kura.

73. Sanduku la kupigia kura.

74. Kituturi.

75. Wakala wa upigaji, kuhesabu na kujumlisha kura.

76. Kutokuwepo wakala.

77. Watu wanaoruhusiwa kuwemo katika kituo cha kupigia kura.

**SEHEMU YA TANO**
**UPIGAJI KURA**

78. Nyakati za kupiga kura.

79. Haki ya muajiriwa.

80. Utaratibu wa Kupiga kura.

81. Kupiga kura kwa kusaidiwa.

82. Kura ya mapema.

83. Malalamiko dhidi ya karatasi ya kura iliyoharibika.

84. Malalamiko kabla, wakati na baada ya upigaji kura.

85. Ufungaji wa kituo cha kupiga kura.

**SEHEMU YA SITA**
**KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO**

86. Kuhesabu kura.

87. Msimamizi wa kituo kuhesabu kura kwa mara ya pili.

88. Kukamilisha kuhesabu kura.

89. Malalamiko baada ya kuhesabu kura.

90. Kura halali.

91. Kura zisizo halali.

92. Kura yenye mgogoro.

93. Msimamizi wa Uchaguzi kufanya majumuisho na kutangaza matokeo.

94. Watu wanaoruhusiwa kuwemo katika kituo cha majumuisho.

95. Msimamizi wa Uchaguzi kufanya majumuisho ya kura kwa mara ya pili.

96. Majumuisho na kutangazwa matokeo ya kura za Rais.

97. Uchapishaji wa matokeo na utoaji wa cheti cha ushindi.

98. Uhifadhi wa Nyaraka.

99. Katazo la kuonesha namna mpiga kura alivyopiga kura.

**SURA YA NNE**
**SEHEMU YA KWANZA**
**UANGALIZI WA UCHAGUZI**

100. Mualiko kwa waangalizi wa uchaguzi.

101. Mipaka ya uangalizi wa uchaguzi.

102. Kipindi cha uangalizi.

103. Ushirikiano na mamlaka zenye uwezo.

104. Utambulisho na vibali kwa waangalizi wa uchaguzi.

105. Wajibu wa waangalizi.

**SEHEMU YA PILI**
**ELIMU YA WAPIGA KURA**

106. Mtaala wa elimu ya mpiga kura.

107. Kibali cha kutoa elimu ya wapiga kura.

108. Kipindi cha kutolewa kwa elimu ya wapiga kura.

**SURA YA TANO**
**UTATUZI WA MIGOGORO NA MALALAMIKO YA UCHAGUZI**

109. Utatuzi wa migogoro ya uchaguzi.

110. Malalamiko ya uchaguzi.

111. Uwasilishaji wa malalamiko ya uchaguzi.

112. Gharama za dhamana.

113. Utaratibu wa Mahkama Kuu inapopokea malalamiko ya uchaguzi.

114. Uwezo wa Mahkama Kuu.

115. Mtu ambaye anaweza kutoa malalamiko ya uchaguzi.

116. Shufaa.

117. Uwezo wa Jaji Mkuu wa kutunga Kanuni.

**SURA YA SITA**
**MAKOSA**

118. Makosa yanayohusiana na uandikishaji.

119. Makosa yanayohusiana na fomu za uteuzi.

120. Makosa yanayohusiana na Kampeni.

121. Kuingia au kuzuia mkutano wa kampeni au hadhara unaofanyika kisheria.

122. Kuchapisha, kubandika na kuweka sehemu ya wazi machapisho bila ruhusa ya Tume.

123. Makosa yanayohusiana na upigaji na kuhesabu kura.

124. Kuvaa au kuonyesha alama au nembo katika kituo cha kupigia kura.

125. Kuharibu uasilia wa nyaraka.

126. Kupiga kura zaidi ya mara moja.

127. Utangazaji wa matokeo kinyume na sheria.

128. Kuzuiya au kuibughudhi Tume, Mjumbe au Afisa wa Tume.

129. Kuingilia upigaji wa kura au uandikishaji.

130. Rushwa.

131. Matumizi ya nguvu.

132. Makosa yanayohusiana na elimu ya wapiga kura.

**SURA YA SABA**
**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA FEDHA**

133. Gharama zitatolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

134. Msamaha wa ushuru wa stempu.

SEHEMU YA PILI
MASHARTI MENGINEYO

135. Matumizi ya teknolojia.

136. Mafunzo.

137. Malalamiko kwa Tume.

138. Kusitisha upigaji kura.

139. Kuakhirisha uchaguzi.

140. Kiapo cha kutunza siri.

141. Kukosa sifa kutokana na hatia ya rushwa au vitendo viovu.

142. Miongozo.

143. Uwezo na mamlaka ya jumla ya Tume.

144. Kanuni, miongozo na taarifa.

145. Kufuta na kubakiza.

**SHERIA NAMBA 4 YA 2018**

**NIMESAINI**

**{DR. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

16 Januari, 2018

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA UCHAGUZI NAM. 11 YA 1984 NA KUTUNGA SHERIA YA UCHAGUZI YA MWAKA 2017 NA MASUALA MENGINE YANAYOHUSIANA NAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

## SURA YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Uchaguzi, 2017 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Kusomwa.

**2.** Sheria hii itasomwa pamoja na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Tafsiri.

**3.** Katika Sheria hii isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:

"Maeneo yanayoruhusiwa" maana yake ni maeneo yote yaliyoruhusiwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa madhumuni ya kubandika mabango ya kampeni ambayo hayahusishi maeneo ya hospitali, skuli, majengo ya ibada na masoko;

"Kitambulisho cha kupigia kura" maana yake ni Kitambulisho cha kupigia kura kilichotolewa kwa mpiga kura kwa mujibu wa kifungu cha 23 cha Sheria hii;

"Afisa Uandikishaji" maana yake ni ofisa aliyeteuliwa na Tume kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha Sheria hii na inajumuisha Msaidizi Afisa Uandikishaji;

"Chama cha Siasa" maana yake ni chama cha siasa kilichosajiliwa kwa masharti ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

"Daftari" maana yake ni Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lililotayarishwa na kuhifadhiwa kwa mujibu wa Sheria hii na inajumuisha sehemu yoyote ya daftari hilo;

"Eneo la Kupigia kura" maana yake ni eneo la uchaguzi ambalo limewekwa kwa mujibu wa kifungu cha 37 cha Sheria hii;

"Eneo la Uchaguzi" maana yake inajumuisha eneo la kupigia kura, katika sehemu ya Uchaguzi, Wadi au Jimbo;

"Eneo la Uandikishaji" maana yake ni eneo la uandikishaji ambalo linatumika kwa ajili ya uandikishaji wapiga kura;

"Gazeti" maana yake ni Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Idara Maalum" maana yake ni Idara zilizoanzishwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar;

"Jimbo" maana yake na inahusisha:

(a) kwa mujibu wa kifungu cha 27(3) cha Katiba ya Zanzibar nzima; au

(b) eneo la uchaguzi lililotangazwa na Tume kwa madhumuni ya uchaguzi wa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

"Karani wa Uandikishaji" maana yake ni mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 8(3) cha Sheria hii;

"Karatasi ya Kura iliyoharibika" maana yake ni karatasi ambayo haikutumika kutokana na kuharibika;

"Karatasi ya Kura" maana yake ni karatasi ya kura iliyotayarishwa na Tume chini ya kifungu cha 72 cha Sheria hii;

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984;

"Kifaa cha kielektroniki" maana yake ni kifaa chochote chenye uwezo wa kutengeneza au kurusha picha mgando au zinazotembea, kurekodi video au kivuli cha aina yoyote na inajumuisha kompyuta, kompyuta ndogo, ipadi, simu ya mkononi, smatifoni, kamera ya kurekodia matukio na kifaa chengine chenye sifa zinazofanana nacho;

"Kituo cha Kupigia Kura" maana yake ni kituo cha kupigia kura kwa mujibu kifungu cha 67 cha Sheria hii;

"Kipindi cha kampeni" maana yake ni kipindi cha kampeni kilichoelezwa katika kifungu cha 62 cha Sheria hii;

"Kura halali" maana yake ni kura ambayo imepigwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 90 cha Sheria hii;

"Kura iliyokataliwa" maana yake ni kura iliyokataliwa na Msimamizi wa kituo chini ya kifungu cha 91 cha Sheria hii;

"Kura ya maoni" maana yake ni utaratibu wa kupeleka suala au hoja kwa wapiga kura ili watoe uamuzi;

"Kura yenye mgogoro" maana yake ni kura ambayo imekataliwa na Mkuu wa Kituo cha kuhesabia kura na kukataliwa kwake kukapingwa na Wakala wa kuhesabu kura kwa mujibu wa kifungu cha 92 cha Sheria hii;

"Mahkama Kuu" maana yake ni Mahakama Kuu ya Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 93 cha Katiba;

"Mgombea" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Tume kugombea katika nafasi ya Urais wa Zanzibar, Ujumbe katika Baraza la Wawakilishi au Udiwani;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Uchaguzi aliyeteuliwa kwa mujibu wa masharti yanayohusiana na Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar;

"Mpiga Kura" maana yake ni mtu yeyote ambaye kwa wakati huu ana sifa ya kupiga kura katika uchaguzi kwa mujibu wa masharti Sheria hii;

"Msaidizi wa Kituo cha Kupigia Kura" maana yake ni mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 68 (b) cha Sheria hii;

"Msimamizi wa Kituo" maana yake ni mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 68(c) cha Sheria hii;

"Msimamizi wa Uchaguzi" maana yake ni ofisa aliyeteuliwa na Tume kwa mujibu wa kifungu cha 36 cha Sheria hii na inajumuisha pia Msaidizi Msimamizi wa Uchaguzi;

"Mtegemezi" maana yake ni mama, baba, mke, mume, babu, bibi, mtoto wa kuzaa wa kike au kiume anayeishi na mpiga kura;

"Mwangalizi" maana yake ni Mtu anayeteuliwa kutoka katika taasisi iliyokubaliwa kwa uangalizi wa Uchaguzi;

“Mwangalizi wa kimataifa” maana yake na inajumuisha mwangalizi kutoka mashirika ya kimataifa, asasi za kimataifa zisizo za kiserikali, Serikali za kigeni na watendaji wake ambao wanatambulika kwa madhumuni ya Sheria hii;

“Mwangalizi wa ndani” maana yake na inajumuisha taasisi za ndani, Asasi zisizo za kiserikali, Mashirika ya kiraia, mashirika na taasisi za kijamii;

“Mwenyekiti” maana yake ni Mwenyekiti wa Tume aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 119(1) cha Katiba na inajumuisha Makamo Mwenyekiti;

“Mzanzibari” maana yake ni raia wa Tanzania mkaazi wa Zanzibar kama alivyotafsiriwa katika Sheria ya Mzanzibari;

“Sheha” maana yake ni Sheha aliyeteuliwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Tawala za Mikoa na inajumuisha Mjumbe wa Kamati ya Ushauri ya Shehia;

“Siku ya Uchaguzi” maana yake ni siku au siku zilizoteuliwa kwa maandishi na Tume kwa ajili ya kuendesha uchaguzi;

“Siku ya Uteuzi” maana yake ni siku iliyopangwa na Tume kwa ajili ya uteuzi wa wagombea;

“Tume” maana yake ni Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliyoanzishwa chini ya masharti ya Katiba;

“Uchaguzi wa Rais” maana yake ni uchaguzi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

“Uchaguzi” maana yake ni Uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi au Madiwani na inahusiana na uchaguzi mdogo na uchaguzi wa marejeo;

“Ufungaji wa Daftari” maana yake ni ufungaji wa daftari kwa kipindi maalumu kilichowekwa na kutangazwa na Tume chini ya kifungu cha 7 cha Sheria hii;

“Uteuzi” maana yake ni uteuzi wa mgombea kwa uchaguzi wa Urais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Serikali za Mtaa na Nafasi za Viti Maalum;

“Wadi” maana yake ni sehemu ya mipaka ya utawala wa Serikali za Mitaa iliyogawiwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar;

“Wakala wa Kuhesabu Kura” maana yake ni mtu aliyeteuliwa kuwa wakala wa kuhesabu kura chini ya kifungu cha 75 cha Sheria hii;

Wakala wa majumuisho" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kuwa wakala wa majumuisho chini ya kifungu cha 75 cha Sheria hii;

"Wakala wa Uandikishaji" maana yake ni mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 15 cha Sheria hii;

"Wakala wa Upigaji wa Kura" maana yake ni mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 75 cha Sheria hii.

Majukumu ya Tume.

**4.**-(1) Kwa mujibu wa masharti ya Katiba, Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na Sheria nyengine zilizopo, majukumu ya Tume yatakuwa yafuatayo:

(a) kusimamia na kuendesha mwenendo mzima wa uchaguzi na kura ya maoni;

(b) kusimamia, kukuza na kuratibu elimu ya wapiga kura;

(c) kuandaa, kutayarisha, kuhifadhi na kuendeleza Daftari;

(d) kufanya mapitio na kuweka mipaka ya majimbo;

(e) kutangaza matokeo ya uchaguzi au kura ya maoni; na

(f) kufanya na kutekeleza kazi na majukumu mengine yote yanayohusiana na uchaguzi au kura ya maoni.

(2) Katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Tume itafanya kazi zake kwa uhuru na haitafuata maelekezo au amri ya mtu au taasisi yoyote.

## SURA YA PILI
## SEHEMU YA KWANZA

## DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA

Kuanzishwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

**5.**-(1) Kutakuwa na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kama litakavyotayarishwa na Tume.

(2) Daftari litakuwa na:

(a) jina kamili;

(b) picha;

(c) tarehe ya kuzaliwa;

(d) sehemu ya makaazi;

(e) nambari ya kujiandikisha;

(f) jinsia;

(g) kituo cha kujiandikisha; na

(h) taarifa nyengine yoyote ambayo ni muhimu kwa kumtambulisha mpiga kura.

(3) Daftari litahifadhiwa Makao Makuu ya Tume.

(4) Tume itaweka katika kila Wilaya nakala ya Daftari la Wapiga Kura kwa kila jimbo la Wilaya husika.

(5) Utaratibu wote wa kuweka daftari, idadi ya madaftari na matumizi yake na namna ya kuweka pingamizi utakuwa kama ambavyo utaelezewa katika Kanuni zitakazotungwa na Tume kwa madhumuni hayo.

Matumizi ya Daftari.

**6.** Daftari litatumika kwa kuendeshea uchaguzi au Kura ya Maoni kwa ajili ya:

(a) kutambua mpiga kura anayestahiki kupiga kura;

(b) kuhakiki wadhamini wa wagombea wakati wa uteuzi;

(c) kuchunguza wapiga kura; au

(d) jambo jengine lolote ambalo Tume itaona linafaa.

Ufungaji wa Daftari.

**7.**-(1) Tume, kwa tangazo litakalochapishwa katika Gazeti, itatangaza kipindi cha kufungwa kwa Daftari siku saba baada ya uteuzi wa wagombea wa uchaguzi au siku thelathini kabla ya kuendeshwa kura ya maoni.

(2) Baada ya kufungwa kwa Daftari chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Tume haitofanya:

(a) uandikishaji wa wapiga kura wapya;

(b) uondoaji wa mpiga kura yeyote katika Daftari;

(c) masahihisho ya taarifa za wapiga kura katika Daftari; au

(d) uhamisho wa taarifa za mpiga kura kutoka eneo moja la uchaguzi kwenda katika eneo jengine la uchaguzi.

(3) Kipindi cha kufungwa kwa Daftari kama kilivyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kitamalizika siku 21 baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi au kura ya maoni.

Maafisa Uandikishaji na Makarani Uandikishaji.

**8.**-(1) Afisa Uchaguzi wa Wilaya kwa nafasi yake atakuwa Afisa Uandikishaji katika Wilaya anayoisimamia.

(2) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, Afisa Uandikishaji atafanya kazi zake kama zilivyowekwa katika Sheria inayohusiana na Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

(3) Afisa Uandikishaji anaweza, kwa mujibu wa sifa na miongozo iliyowekwa na Tume, kuteuwa Makarani wa Uandikishaji kama anavyoona inafaa.

(4) Kwa mujibu wa miongozo hiyo ya Tume, Afisa Uandikishaji anaweza, mara kwa mara, kutoa maelekezo kwa Karani wa Uandikishaji ambaye atatekeleza majukumu na uwezo aliopewa au kukasimiwa na Afisa Uandikishaji.

Majukumu ya Karani wa Uandikishaji.

**9.** Karani wa Uandikishaji katika kutekeleza kazi zake katika kituo cha uandikishaji atahakikisha kuwa:

(a) kituo cha uandikishaji kimepangwa vizuri;

(b) kuna vifaa vya uandikishaji vya kutosha;

(c) kuna usalama na mazingira mazuri ya kufanyia kazi;

(d) waombaji wenye sifa tu ndio wanaoandikishwa;

(e) fomu za uandikishaji zinajazwa kwa usahihi; na

(f) uandikishaji unafanyika kwa mujibu wa sheria, Kanuni zinazohusiana na uandikishaji na miongozo ya Tume.

Uwezo wa Karani wa Uandikishaji.

**10.** Karani wa Uandikishaji atakuwa na dhamana ya shughuli za uandikishaji katika kituo na atakuwa na uwezo wa kufanya yafuatayo:

(a) kumuamrisha Afisa wa Polisi katika kituo kuhakikisha uwepo wa utiifu wa sheria na kufuatwa kwa maelekezo;

(b) kumuamrisha mtu yeyote kuondoka katika kituo baada ya kujiridhisha kuwa uwepo wa mtu huyo unahatarisha kazi ya uandikishaji;

(c) kumzuia mwombaji au mtu mwengine yeyote kuingia katika kituo cha uandikishaji na zana au kifaa kisichoruhusiwa;

(d) kuzuia matumizi ya vifaa vya kielektroniki katika kituo cha uandikishaji isipokuwa kwa wale watu walioruhusiwa tu; na

(e) kumwandikisha au kutomwandikisha muombaji kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na miongozo ya Tume.

## SEHEMU YA PILI
## UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA

Wakati na eneo la Uandikishaji.

**11.**-(1) Tume kwa tangazo lililochapishwa katika Gazeti, itapanga na kutangaza wakati na pahala pa uandikishaji wa wapiga kura kama itakavyoona inafaa.

(2) Mtu yeyote ambaye ana sifa ya kuandikishwa kuwa mpiga kura katika eneo la uandikishaji na hajaandikishwa katika Daftari, anaweza kwenda yeye mwenyewe katika eneo la uandikishaji kwa ajili ya kuandikishwa kama ambavyo Tume itaelekeza.

Sifa za kuandikishwa.

**12.**-(1) Mtu atakuwa na sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura ikiwa:

(a) ni Mzanzibari;

(b) amefikia umri wa miaka kumi na nane;

(c) anacho na ataonesha Kitambulisho chake cha Mzanzibari Mkaazi kilichotolewa chini ya Sheria zinazohusiana na kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi;

(d) ana makaazi ya kudumu na amekuwa akiishi katika Jimbo hilo kwa kipindi cha miezi 36 mfululizo;

(e) jina lake halimo katika Daftari la Jimbo lolote lile; na

(f) hajazuiwa kuandikishwa kuwa mpiga kura na sheria nyengine yoyote ile.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1)(d) cha kifungu hiki, mtu atachukuliwa kuwa ana sifa za kuandikishwa katika Jimbo ikiwa:

(a) ana ndoa na anaishi katika jimbo hilo mradi mwenza wake wa ndoa ni mkaazi wa kudumu wa eneo la uandikishaji;

(b) anaishi katika jimbo kutokana na sababu za ajira; au

(c) ni mtegemezi wa mmoja au watu wote ambao wameelezwa katika aya ya (a) na (b) ya kifungu hiki.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha 2(b) cha kifungu hiki, mtu atakuwa na sifa zinazotokana na misingi ya ajira iwapo:

(a) ni Afisa wa Usalama ambaye amepata uhamisho wa kikazi na inahusisha wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Afisa Usalama wa Taifa, Jeshi la Polisi Tanzania na Idara Maalum;

(b) ni mfanyakazi wa Serikali au mwajiriwa wa shirika la kimataifa ambaye amepata uhamisho kutokana na kazi zake;

(c) ni mwanamke aliyeolewa au mwanamme aliyeowa mtu ambaye ana sifa ya kikazi aliyehamia katika eneo jengine kutokana na uhamisho wa mume au mke wake;

(d) ni mtegemezi wa mtu mwenye sifa ya kikazi ambaye amekidhi masharti ya aya ya (a) au (b) au (c) ya kifungu hiki.

(4) Mtu ambaye kwa madhumuni ya sifa ya ukaazi, hana sifa ya kuandikishwa katika jimbo analoishi sasa, anaweza kurejea katika jimbo la zamani na kuandikishwa kuwa mpiga kura na atakuwa na haki ya kuandikishwa katika jimbo hilo.

Taratibu za Uandikishaji.

**13.**-(1) Kila Mzanzibari aliyetimia umri wa miaka kumi na nane, isipokuwa awe amezuilika kutokana na Sheria hii au sheria nyengine yoyote, atakuwa na haki ya kuandikishwa kuwa mpiga kura chini ya masharti ya Sheria hii.

(2) Afisa Uandikishaji kwa kufuata miongozo ya Tume, atamuandikisha mtu mwenye sifa ambaye ataomba na kwenda mwenyewe binafsi mbele yake au mbele ya Karani wa Uandikishaji kwa ajili ya kuandikishwa.

(3) Afisa Uandikishaji au Karani wa Uandikishaji baada ya kuridhika na nyaraka na sifa za muombaji, atamwandikisha muombaji huyo na atampatia risiti kuthibitisha kukubaliwa maombi yake.

Sheha kuwa wakala wa uandikishaji kwa wadhifa wake.

**14.**-(1) Sheha kutokana na wadhifa wake atakuwa ni Wakala wa Uandikishaji wa Tume katika shehia yake.

(2) Kila Sheha au mwakilishi wake katika Shehia ambayo kituo cha uandikishaji kimeanzishwa, atashirikiana na Afisa Uandikishaji au Karani wa Uandikishaji kuhakikisha usimamizi mzuri wa sheria na kanuni zinazohusiana na Uandikishaji wa wapiga kura katika kituo.

Wakala wa Uandikishaji.

**15.**-(1) Kila chama cha siasa kinaweza, wakati wa uandikishaji kuteuwa mwanachama wake mmoja ambaye ameandikishwa au ana sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura katika shehia, kuwa wakala wa uandikishaji katika shehia hiyo.

(2) Majina na anuani za Mawakala wa Uandikishaji walioteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki pamoja na vituo vya uandikishaji ambavyo wamepangiwa kazi, vitawasilishwa kwa Afisa Uandikishaji si zaidi ya siku saba kabla ya kuanza siku ya uandikishaji au ndani ya muda mfupi kama Tume itakavyoruhusu.

(3) Wakala wa uandikishaji aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki atakiwakilisha chama chake na atasaidia kugundua wanaojifananisha.

(4) Wakala wa Uandikishaji atashirikiana na Afisa Uandikishaji na Karani wa Uandikishaji kuhakikisha utekelezaji mzuri wa Sheria na Kanuni zinazohusiana na uandikishaji.

(5) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kila wakala wa uandikishaji anawajibika kuwepo wakati wa kufunguliwa kwa kituo cha uandikishaji ambacho ameteuliwa.

Isipokuwa kwamba kutokuwepo kwa Wakala wa Uandikishaji katika kituo hakutasimamisha kazi za uandikishaji.

Watu wanaoruhusiwa katika kituo cha uandikishaji.

**16.** Watu wafuatao wataruhusiwa kuwemo katika kituo cha uandikishaji:

(a) Afisa Uandikishaji;

(b) Karani wa Uandikishaji;

(c) Sheha;

(d) Wakala wa Uandikishaji;

(e) Muombaji;

(f) Mtu anayemsaidia muombaji mwenye mahitaji maalumu;

(g) Mwangalizi aliyeidhinishwa kwa maandishi na Tume;

(h) Mjumbe wa Tume;

(i) Mkurugenzi wa Uchaguzi;

(j) Askari Polisi au Afisa yeyote wa usalama atakayekuwepo kituoni kwa ulinzi; au

(k) Mtu mwengine yeyote atakayeidhinishwa na Tume.

Kukataliwa kwa maombi ya kuandikishwa.

**17.**-(1) Endapo Karani wa Uandikishaji atayakataa maombi ya kuandikishwa ya muombaji, kulingana na masharti ya sehemu hii, atajaza maelezo katika fomu maalumu iliyowekwa na kumpatia muombaji inayoelezea sababu za kukataliwa kuandikishwa.

(2) Iwapo muombaji hakuridhika na uamuzi wa Karani wa Uandikishaji, atawasilisha malalamiko yake kwa Afisa Uandikishaji ambaye atayatolea uamuzi malalamiko hayo ndani ya siku saba.

(3) Iwapo muombaji hakuridhika na uamuzi wa Afisa Uandikishaji, atakata Rufaa kwa Tume ndani ya siku saba.

(4) Rufaa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki itafunguliwa na kuamuliwa ndani ya siku kumi na nne baada ya uamuzi wa Afisa Uandikishaji.

(5) Uamuzi wa Tume juu ya maswala ya uandikishaji uliofanywa chini ya kifungu hiki utakuwa wa mwisho na hautojadiliwa na mtu au taasisi yoyote.

Uamuzi wa Tume juu ya Rufaa.

**18**. Endapo jina la mtu yeyote:

(a) limeamuliwa na Tume liingizwe katika orodha ya walioomba kuandikishwa; au

(b) limeamuliwa lisiingizwe katika orodha ya walioomba kuandikishwa,

Afisa wa Uandikishaji baada ya kupata maelekezo ya Tume atachukuwa hatua ya kuliingiza au kutoliingiza jina hilo, kwa kadiri itakavyokuwa katika Daftari.

Kuweka Wazi Orodha za Waombaji.

**19.**-(1) Afisa Uandikishaji, baada ya kukamilisha kuandikisha na kwa kufuata miongozo ya Tume, ataweka wazi au ataagiza kuwekwa wazi kwa siku saba orodha za waombaji wapya katika kila kituo cha uandikishaji au katika sehemu itakayoelekezwa na Tume.

(2) Mpiga kura yeyote au muombaji anaweza kuchunguza orodha ya wapiga kura iliyowekwa wazi kwa madhumuni ya kuthibitisha kama yumo, kuangalia usahihi wa taarifa zake au kuziwekea pingamizi taarifa za muombaji yeyote asiyekuwa na sifa za kuwemo katika orodha ya waombaji.

Malalmiko dhidi ya orodha iliyowekwa wazi.

**20.**-(1) Muombaji yeyote ambaye baada ya uchunguzi wa orodha amegundua kuwa jina lake halimo au taarifa zake si za kweli, anaweza kuomba kwa Afisa Uandikishaji kwa kujaza fomu iliyoandaliwa kuwa jina au taarifa zake ziingizwe katika orodha au zifanyiwe masahihisho.

(2) Afisa Uandikishaji baada ya kupokea malalamiko na baada ya uchunguzi akagundua kuwa:

(a) muombaji ana haki ya kuwemo katika Daftari, atamwandikisha muombaji huyo;

(b) taarifa za muombaji hazijanukuliwa kwa usahihi, atazifanyia masahihisho taarifa hizo; au

(c) muombaji hana haki kwa mujibu wa maelezo ya kifungu kidogo cha (2)(a) na (b) cha kifungu hiki, atakataa maombi ya muombaji huyo na ataelezea sababu ya kukataa kwake kwa kujaza maelezo katika fomu iliyoandaliwa.

(3) Endapo muombaji hatoridhika na maamuzi ya Afisa Uandikishaji, atakata rufaa kwa Tume ndani ya siku saba.

Pingamizi ya Muombaji.

**21.**-(1) Mtu yeyote ambaye jina lake limo katika Daftari au katika orodha ya waombaji wa eneo husika la uandikishaji, anaweza kuliwekea pingamizi jina la mtu mwengine yeyote ambalo limo katika orodha ya wapiga kura kutokana na sababu kuwa mtu huyo hana sifa au hastahiki tena kuwemo katika Daftari la eneo hilo.

(2) Utaratibu wa kuweka pingamizi, muda, namna ya kuweka dhamana na pahala pa kusikiliza pingamizi vitakuwa kama vitakavyoelezewa katika Kanuni chini ya Sheria hii.

Kuingizwa katika Daftari.

**22.** Afisa Uandikishaji baada ya kuridhika kukamilika kwa taratibu za kumwandikisha muombaji, ataziingiza taarifa za mwombaji huyo katika Daftari na kuwa mpiga kura.

Kitambulisho cha Mpiga kura.

**23.**-(1) Kutakuwa na kitambulisho cha mpiga kura kitakachotayarishwa na Tume kulingana na sifa za kujiandikisha.

(2) Afisa Uandikishaji kwa kufuata miongozo ya Tume, atatoa vitambulisho kwa wapiga kura walioandikishwa.

Kitambulisho kilichopotea au kuharibika.

**24.**-(1) Pale ambapo Kitambulisho cha Mpiga kura kimepotea, kimechafuka au kuharibika, mpiga kura anaweza kuomba yeye mwenyewe kwa Afisa Uandikishaji kupatiwa kitambulisho kipya cha kupigia kura.

(2) Endapo Afisa Uandikishaji ataridhika na maombi yaliyofanywa kulingana na maelekezo ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atampatia muombaji kitambulisho kipya cha kupigia kura baada ya muombaji kulipia ada iliyowekwa na kukabidhi kitambulisho kilichochafuka au kuharibika.

(3) Maombi yaliyofanywa chini ya kifungu hiki yatawasilishwa kwa tamko katika fomu maalum iliyotayarishwa kwa mujibu wa Kanuni zilizotayarishwa.

SEHEMU YA TATU
UKAGUZI WA DAFTARI

Ukaguzi wa Daftari.

**25.**-(1) Mtu yeyote aliyeandikishwa kuwa mpiga kura kwa maombi yaliyofanywa kwa Afisa Uandikishaji, anaweza kukagua Daftari la kituo chake alichoandikishwa ndani ya Wilaya.

(2) Utaratibu wa kukagua Daftari utakuwa kama ulivyoelezewa katika Kanuni zilizotayarishwa kwa mujibu wa Sheria hii.

Malalamiko dhidi ya Daftari.

**26.**-(1) Mpiga kura aliyeandikishwa anaweza, baada ya kulikagua Daftari na akagundua kuwa jina lake halimo au taarifa zake haziko sawa, kuomba kwa Afisa Uandikishaji kwa kutumia fomu iliyoandaliwa kutaka jina lake au taarifa zake kuingizwa au kufanyiwa masahihisho.

(2) Afisa Uandikishaji, anaweza baada ya kupokea maombi na kuridhika kwamba muombaji ana haki ya kuingizwa katika Daftari au taarifa za muombaji hazikuandikwa kwa usahihi, atamwandikisha muombaji huyo au kusahihisha taarifa zake kama inavyostahiki.

(3) Afisa Uandikishaji atakataa kwa kupitia fomu maalum, maombi ya muombaji yaliyofanywa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki na kutoa sababu zake, akiona kuwa madai ya muombaji ya kutaka kuingizwa katika Daftari au kusahihishiwa taarifa zake hayana msingi.

Pingamizi dhidi ya mtu aliye katika Daftari.

**27.**-(1) Mpiga kura yeyote ambaye jina lake limo katika Daftari la eneo la kupigia kura, anaweza kuliwekea pingamizi jina la mtu yeyote aliyemo katika Daftari kutokana na kuwa mtu huyo hana sifa au hana tena sifa za kuandikishwa katika eneo hilo.

(2) Utaratibu wa kuweka pingamizi, wakati, namna ya kuweka dhamana na pahala pa kusikiliza pingamizi utakuwa kama utakavyoelezwa katika Kanuni zitakazotayarishwa na Tume.

Uchunguzi na maamuzi ya Afisa Uandikishaji.

**28.**-(1) Afisa Uandikishaji haraka iwezekanavyo, atafanya uchunguzi kuhusiana na pingamizi zote zilizowekwa.

(2) Afisa Uandikishaji katika kipindi kisichopungua siku kumi na nne, atatoa taarifa ya maandishi juu ya tarehe, muda na pahala ambapo pingamizi itasikilizwa kwa kila muweka pingamizi na kwa mtu aliyewekewa pingamizi.

(3) Mtu yeyote ambaye anahusika au ameathiriwa na uchunguzi wa suala hilo, anaweza kujitokeza na kusikilizwa yeye binafsi au mtu yeyote ambaye atamuidhinisha kwa maandishi kwa niaba yake kwa Afisa Uandikishaji.

(4) Afisa Uandikishaji atasikiliza pingamizi iliyowasilishwa na kuamua kwa mujibu wa utaratibu na:

(a) atafuta au kuelekeza kufutwa jina la mtu huyo kutoka katika Daftari iwapo ataridhika kuwa sifa za anayepingwa hazikuthibitishwa; au

(b) atabakisha au kuliingiza kama inavyowezekana au kuelekeza kubakishwa au kuingizwa jina la mtu aliyewekewa pingamizi katika Daftari, iwapo ataridhika kuwa sifa za mtu huyo zimethibitishwa.

(5) Endapo muweka pingamizi au mtu yeyote aliyeidhinishwa kwa maandishi kwa niaba yake atashindwa kutokea katika tarehe iliyopangwa kwa uchunguzi juu ya pingamizi, au atakuwepo lakini akashindwa kutoa ushahidi wa pingamizi yake na kumridhisha Afisa Uandikishaji, Afisa Uandikishaji atalibakisha au ataelekeza kubakishwa jina la mpiga kura katika Daftari au kama itakavyokuwa, hatochukua hatua zozote kulifanyia masahihisho Daftari.

(6) Endapo pingamizi iliyowekwa na mtu yeyote imekataliwa, Afisa Uandikishaji anaweza kutoa amri kwa maandishi kumtaka mweka pingamizi kumlipa mtu ambaye amemuwekea pingamizi fidia ya kiasi cha fedha kama itakavyoelekezwa na Tume.

(7) Endapo pingamizi itakataliwa na Afisa Uandikishaji na ikawa ana maoni kuwa pingamizi iliwekwa bila ya kuwa na sababu za msingi, dhamana itakayowekwa itachukuliwa na Serikali au kurejeshwa kwa mweka pingamizi kwa amri itakayotolewa na Afisa Uandikishaji.

(8) Iwapo muombaji hakuridhika na uamuzi wa Afisa Uandikishaji atakata rufaa kwa Tume ndani ya siku saba.

(9) Rufaa chini ya kifungu kidogo cha (8) cha kifungu hiki itawasilishwa na kutolewa uamuzi ndani ya siku kumi na nne tangu kutolewa maamuzi na maamuzi ya Tume yatakuwa ya mwisho na hayatojadiliwa.

## SEHEMU YA NNE
## UENDELEZAJI WA DAFTARI

Uhamisho wa taarifa za Mpiga Kura.

**29.**-(1) Pale mpiga kura katika eneo moja la uchaguzi amekuwa mkaazi wa kudumu katika eneo jengine la uchaguzi, anaweza kuomba kwa Afisa Uandikishaji kuhamishiwa taarifa zake kutoka eneo la zamani kwenda katika eneo la sasa la kupigia kura.

(2) Endapo Afisa Uandikishaji ataridhika kuwa muombaji ni mpiga kura na ni mkaazi wa kudumu wa eneo husika la uchaguzi ambalo anaomba kuhamishiwa taarifa zake, atahamisha taarifa za mpiga kura huyo katika eneo la uchaguzi analoomba.

Isipokuwa kwamba, uhamisho wa taarifa za mpiga kura huyo utakamilika tu baada ya muombaji kuidhinishwa na Sheha wa Shehia ambayo muombaji ametimiza sifa za uhamisho na amekabidhi kitambulisho chake cha zamani.

(3) Endapo Afisa Uandikishaji amehamisha taarifa za muombaji kama ilivyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atafuta kitambulisho cha kupigia kura atakachokabidhiwa na muombaji.

(4) Afisa Uandikishaji baada ya kukamilisha kuhamisha taarifa za muombaji chini ya kifungu hiki na baada ya kulipwa ada iliyowekwa kwa mujibu wa Kanuni iliyotungwa chini ya Sheria hii, atampatia au ataelekeza kupatiwa kitambulisho kipya cha kupigia kura.

Maombi ya kubadilisha taarifa za mpiga kura aliyeandi-kishwa.

**30.** Afisa Uandikishaji inapotokezea kuwa taarifa za mpiga kura katika Daftari zinahitaji kufanyiwa masahihisho kwa sababu yoyote ile ya kisheria na baada ya kupokea maombi ya kufanya masahihisho toka kwa mpiga kura, atafanya au ataagiza kufanyiwa masahihisho yote muhimu katika Daftari na atamuarifu Mkurugenzi.

Isipokuwa kwamba, hakuna kitambulisho kipya cha kupigia kura kitakachotolewa chini ya kifungu hiki mpaka muombaji atakapokabidhi kitambulisho chake cha zamani cha kupigia kura au kumridhisha Afisa Uandikishaji kuwa kimepotea na kulipia ada atakayoelekezwa.

Kumuondoa mpiga kura asiyekuwa na sifa.

**31.**-(1) Afisa Uandikishaji, kwa kufuata miongozo ya Tume, atafanya uchunguzi ili kuthibitisha taarifa za wapiga kura wanaohitajika kuondolewa katika Daftari.

(2) Afisa Uandikishaji wakati wa kufanya uchunguzi wake anaweza kutumia taarifa kutoka katika vyombo vifuatavyo:

(a) taasisi inayohusika na maswali ya vizazi na vifo;

(b) Sheha;

(c) taasisi inayohusika na masuala ya uhamiaji;

(d) taasisi inayohusika na Usajili wa Wakaazi na Vitambulisho;

(e) taasisi nyengine yoyote kwa mujibu wa mwongozo wa Tume; au

(f) jamaa wa muhusika.

(3) Kuhusiana na vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki, Afisa Uandikishaji anaweza kumwondoa mpiga kura yeyote ambaye hana sifa kwa mujibu wa maelekezo chini ya Kanuni iliyotungwa na Tume.

Kuweka wazi orodha ya wapiga kura wanaohamisha taarifa na waliopoteza sifa.

**32.** Afisa Uandikishaji atatayarisha na kuweka wazi orodha ya wapiga kura waliohamisha taarifa au kupoteza sifa za kuwa wapiga kura kwa siku saba katika eneo la wazi la ofisi ya Wilaya au eneo jengine lolote lililoamuliwa na Tume kwa ajili ya pingamizi kama zitakuwepo.

Kubadili jina.

**33.** Mtu aliyeandikishwa kuwa mpiga kura na jina lake likabadilika kwa sababu ya kuolewa au kwa njia nyengine, iwapo hajafutwa kupiga kura chini ya kifungu cha 31 cha Sheria hii, atakuwa na haki ya kupiga kura kwa kutumia jina ambalo ameandikishwa.

## SURA YA TATU
## SEHEMU YA KWANZA
## UCHAGUZI MKUU

Uchaguzi Mkuu.

**34.**-(1) Kwa mujibu wa masharti ya Katiba, kutakuwa na Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar ambao utafanyika kila baada ya miaka mitano.

(2) Uchaguzi Mkuu chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki utajumuisha uchaguzi wa:

(a) Rais;

(b) Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi; na

(c) Madiwani.

(3) Tume, kupitia tangazo lililochapishwa katika Gazeti, itatangaza tarehe ya Uchaguzi Mkuu ambayo haitapungua siku sitini na isiyozidi siku tisini kuanzia siku ya kuvunjwa kwa Baraza la Wawakilishi.

(4) Tangazo lililochapishwa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki litajumuisha:

(a) Tarehe ya uchaguzi;

(b) Kipindi cha kuchukuwa na kurejesha fomu ya uteuzi;

(c) Siku ya uteuzi;

(d) Kipindi cha kampeni; na

(e) Kupiga, kuhesabu kura na kutangaza matokeo.

(5) Tume inaweza, pale mazingira yanapohitaji, kutangaza tarehe tofauti za kufanyika Uchaguzi Mkuu katika Majimbo tofauti.

Watu wenye haki ya kupiga kura.

**35.**-(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 7(2) cha Katiba, kila mtu aliyeandikishwa kuwa mpiga kura chini ya Sheria hii atakuwa na haki ya kupiga kura katika uchaguzi.

(2) Mpiga kura aliyeandikishwa anaweza kupiga kura katika kituo cha kupigia kura alichopangiwa katika eneo la kupigia kura ambalo ameandikishwa katika jimbo.

(3) Tume kupitia Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii, inaweza kutoa maelekezo na kuweka mazingira ambayo mpiga kura kwa Uchaguzi wa Rais, anaweza kuruhusiwa kupiga kura mbali na kituo ambacho amepangiwa.

Msimamizi, Msaidizi Msimamizi wa uchaguzi na watendaji wa vituo.

**36.**-(1) Afisa wa Uchaguzi wa Wilaya atakuwa, kwa mujibu wa nafasi yake na masharti ya Sheria inayohusiana na Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Msimamizi wa Uchaguzi wa Majimbo ya Wilaya anayoisimamia.

(2) Tume, kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itateua kwa kila uchaguzi katika kila jimbo Msaidizi Msimamizi wa Uchaguzi kulingana na sifa zilizowekwa na Tume, kwa madhumuni ya kusaidia uendeshaji wa uchaguzi katika jimbo.

(3) Msimamizi wa Uchaguzi anaweza, kwa maelekezo ya Mkurugenzi, kuajiri watendaji wa vituo vya kupigia kura kutokana na mahitaji ya kuweza kusimamia uchaguzi katika jimbo.

(4) Msimamizi wa Uchaguzi anaweza, mara kwa mara, kutoa maelekezo kwa Msaidizi Msimamizi wa Uchaguzi kutekeleza majukumu au uwezo aliopewa au alionao na maelezo yanayohusiana na Msimamizi wa Uchaguzi yatachukuliwa kuwa yamejumuisha maelezo kwa Msaidizi Msimamizi wa Uchaguzi.

(5) Msimamizi wa Uchaguzi kabla ya kuanza utekelezaji wa majukumu yake chini ya Sheria hii, atakula kiapo cha kutunza siri na uadilifu mbele ya Hakimu wa Mkoa katika fomu iliyotayarishwa.

Maeneo ya kupigia kura.

**37.**-(1) Tume italigawanya kila jimbo katika maeneo ya kupigia kura na itatangaza katika Gazeti taarifa inayobainisha maeneo hayo ya kupigia kura.

(2) Pale ambapo mipaka ya majimbo imebadilika au katika hali yoyote ile ambayo Tume imeona inafaa kufanya hivyo, inaweza kubadilisha idadi na maeneo ya kupigia kura katika jimbo na baada ya mabadiliko hayo itachapisha katika Gazeti tangazo linaloainisha mabadiliko hayo.

(3) Pale ambapo zimetokea athari za mabadiliko ya kuanzishwa au kubadilishwa kwa mipaka ya jimbo, eneo moja la kupigia kura katika jimbo limeingia katika eneo la

jimbo jengine, Tume inaweza kutangaza kwamba, eneo hilo limesita kuwa eneo la kupigia kura katika jimbo la awali na litakuwa ndani ya jimbo ambalo liko sasa.

(4) Tume inaweza, kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, kutoa vitambulisho vipya vya kupigia kura kwa wapiga kura wa eneo lililoathirika na mabadiliko ya mipaka.

Taarifa ya Uchaguzi.

**38.**-(1) Msimamizi wa uchaguzi, kwa kuzingatia taarifa ya uchaguzi iliyochapishwa na Tume chini ya kifungu cha 34(3) cha Sheria hii na katika kipindi cha siku kumi na nne kabla ya uchaguzi, atatoa taarifa ya uchaguzi katika jimbo kama anavyoona inafaa juu ya mambo yafuatayo:

(a) siku na kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, muda wa kuanza na kufunga vituo vya kupigia kura;

(b) anuani za maeneo na vituo vya kupigia kura;

(c) idadi ya wapiga kura iliyopangwa kwa kila eneo na kituo cha kupigia kura; na

(d) jina kamili, anuani, kazi na nembo ya chama cha kila mgombea.

(2) Siku iliyoteuliwa kupiga kura chini ya masharti ya aya (a) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki katika eneo lolote la kupigia kura, inaweza kuwa tofauti na siku iliyoteuliwa kwa eneo jengine la kupigia kura katika jimbo moja.

Isipokuwa kwamba siku ya uchaguzi katika jimbo itakuwa siku ya upigaji kura katika angalau eneo moja la kupigia kura katika jimbo.

(3) Endapo Msimamizi wa Uchaguzi, baada ya kushauriana na Mkurugenzi, ameteuwa siku ya upigaji kura kwa eneo la upigaji kura chini ya masharti ya kifungu hiki, anaweza kutoa taarifa hiyo katika jimbo kama atakavyoona inafaa, kubadilisha siku ya upigaji kura iliyoteuliwa kwa eneo lolote la uchaguzi, na baada ya hapo upigaji kura utafanyika katika eneo hilo katika tarehe iliyoainishwa kwenye taarifa hiyo.

(4) Kwa madhumuni ya aya (a) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, isipokuwa kama Tume imeelekeza vyenginevyo, wakati wa kuanza upigaji kura utakuwa saa moja kamili asubuhi na wakati wa kufunga upigaji kura utakuwa saa kumi kamili jioni au muda wa mapema zaidi kama itakavyoainishwa katika tangazo.

Ubandikaji wa Daftari katika eneo la kupigia kura.

**39.** Msimamizi wa Uchaguzi atabandika, siku saba kabla ya upigaji kura, Daftari katika sehemu ya wazi ya eneo la kupigia kura ili kuwawezesha wapiga kura kufahamu taarifa zao na vituo vyao vya kupigia kura.

Uchaguzi mdogo.

**40.** -(1) Kutakuwa na uchaguzi mdogo utakaofanyika kutokana na mambo yafuatayo:

(a) Kwa upande wa Rais, utafanyika kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha (34) cha Katiba;

(b) kwa upande wa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, utafanyika kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 71 cha Katiba; na

(c) kwa upande wa Diwani utafanyika kutokana na kifo, kujiuzulu au sababu nyengine yoyote ambayo itamfanya Diwani kupoteza sifa ya kuwa Diwani.

(2) Tume, mara baada ya kupokea taarifa rasmi kutoka katika mamlaka inayohusika, kama ilivyoainishwa katika kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, itatangaza siku ya uteuzi ambayo haitazidi siku thelathini kwa ajili ya uchaguzi mdogo.

(3) Iwapo uchaguzi mdogo umepangwa kufanyika, siku ya uteuzi haitakuwa chini ya miezi minne na haitakuwa zaidi ya miezi kumi na mbili baada ya kutokea kwa tukio lililopelekea uchaguzi mdogo kufanyika.

(4) Mamlaka inayohusika katika kifungu hiki maana yake ni Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa nafasi iliyowazi ya Rais au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Waziri anayehusika na masuala ya Serikali za Mitaa kwa kiti kilichowazi cha Diwani.

(5) Bila ya kujali masharti ya vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki, Tume inaweza kwa kuzingatia sababu za msingi ambazo zimepelekea kutokea kwa jambo lililozuia kufanyika kwa uchaguzi mdogo katika siku iliyoteuliwa, kuifuta siku iliyoteuliwa awali na kuteua siku nyengine kwa ajili ya uchaguzi huo ambayo itakuwa siku iliyo ndani ya muda ulioelezwa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki.

(6) Hakutokuwa na uchaguzi mdogo katika miezi kumi na mbili ya mwisho wa maisha ya Baraza la Wawakilishi.

Uchaguzi wa marudio.

**41.**-(1) Pale ambapo Tume itaridhika, kabla ya kutangaza matokeo ya uchaguzi kwamba kulikuwa na kutofuatwa kwa taratibu, matumizi mabaya au ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi; au

(2) Pale ambapo kura za wagombea waliopata idadi ya kura za juu imelingana.

Tume ama itasimamisha au kufuta uchaguzi au sehemu yoyote ya Uchaguzi na itatangaza siku nyengine ya kurudia uchaguzi.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, uchaguzi wa marudio maana yake ni utaratibu wa upigaji kura kwa kuzingatia wagombea wale wale walioteuliwa katika uchaguzi kabla ya uchaguzi kufutwa au kusimamishwa.

## SEHEMU YA PILI
## UTEUZI WA WAGOMBEA

Siku ya uteuzi.

**42.**-(1) Tume itateuwa siku ya uteuzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar ambayo haitapungua siku tano na haitazidi siku ishirini na moja baada ya kuvunjwa kwa Baraza la Wawakilishi.

(2) Uteuzi wa wagombea utafanyika saa ishirini nne baada ya siku ya mwisho ya kurejesha fomu za uteuzi; ambapo:

(a) Tume itateuwa Wagombea wa Urais; na

(b) Msimamizi wa Uchaguzi atateuwa wagombea wa Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

(3) Uteuzi wa wagombea utazingatia masharti ya Katiba, Sheria hii, taarifa za mgombea na pingamizi zilizowekwa kama zipo, katika fomu ya uteuzi.

(4) Mgombea ambaye atashindwa kutekeleza masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, hatateuliwa na Tume au Msimamizi wa Uchaguzi, kwa kadiri itakavyokuwa.

Sifa za Mgombea wa Urais.

**43.** Kwa kuzingatia masharti ya Katiba, mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mgombea wa Urais iwapo:

(a) ni Mzanzibari wa kuzaliwa;

(b) ametimia umri wa miaka arobaini;

(c) ametimiza masharti ya kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi; na

(d) ni mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa ambacho kimesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa.

Sifa za Kugombea Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi.

**44.** Kwa kuzingatia masharti ya Katiba, mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa mgombea wa Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi iwapo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ametimia umri wa miaka ishirini na moja;

(c) ameandikishwa au ana sifa za kuandikishwa katika jimbo kama mpiga kura kwa uchaguzi wa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi;

(d) anaweza kusoma, lakini ikiwa ana ulemavu wa uoni au aina nyengine ya ulemavu wa viungo anaweza kuzungumza lugha ya Kiswahili;

(e) ni mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa ambacho kimesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa; na

(f) hazuiliki kugombea uchaguzi chini ya masharti ya Katiba au sheria nyengine.

Siza za Mgombea wa Udiwani.

**45.** Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa mgombea wa Udiwani iwapo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ametimia umri wa miaka ishirini na moja;

(c) ameandikishwa au ana sifa za kuandikishwa katika jimbo kama mpiga kura;

(d) anaweza kusoma, lakini ikiwa ana ulemavu wa uoni au aina nyengine ya ulemavu wa viungo, anaweza kuzungumza lugha ya Kiswahili;

(e) ni mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa ambacho kimesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa;

(f) ni mkaazi wa kawaida katika eneo la mamlaka ya Serikali ya Mtaa; na

(g) hazuiliki kugombea uchaguzi chini ya masharti ya Katiba au sheria nyengine.

Fomu ya Uteuzi.

**46.-**(1) Tume kwa madhumuni ya uchaguzi, itaandaa fomu ya uteuzi katika mfumo ambao inaona unafaa kumtambua na kuzijua sifa za mgombea.

(2) Fomu ya uteuzi iliyoelezwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itajumuisha yafuatayo:

(a) taarifa za mgombea na chama chake;

(b) majina ya wadhamini wanaohitajika; na

(c) hati ya kiapo katika fomu iliyoandaliwa na kusainiwa na mgombea mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu kwa mgombea wa Urais na Hakimu kwa mgombea wa Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi au Udiwani.

Uchukuwaji na Urejeshaji wa Fomu za wagombea.

**47.**-(1) Tume kwa madhumuni ya uchaguzi itatangaza siku ya kuchukuwa na kurejesha fomu za uteuzi ambayo haitazidi siku ishirini na moja kutoka siku ya uteuzi.

(2) Kila chama cha siasa kinachokusudia kugombea uchaguzi kitawasilisha kwa Tume au Msimamizi wa Uchaguzi, kwa kadiri itavyokuwa, jina la mgombea wake na kuainisha siku na wakati wa kuchukuwa fomu.

(3) Tume au Msimamizi wa Uchaguzi, kwa kadiri itavyokuwa, baada ya kupokea majina ya wagombea waliopendekezwa kuchukuwa fomu, itaandaa ratiba ya uchukuwaji wa fomu na kuifanyia kazi.

(4) Mgombea aliyechukua fomu ya uteuzi chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki atairudisha wakati wowote kabla ya saa kumi za jioni za siku ya mwisho ya urejeshaji wa fomu pamoja na picha za mgombea kama katika kanuni za Tume itakavyoelekezwa.

(5) Tume itaweka ada ya uchukuwaji wa fomu ya uteuzi ambayo haitarejeshwa.

Wadhamini wa Mgombea.

**48.** Mgombea atateuliwa kihalali kugombea:

(a) Uchaguzi wa Rais iwapo atadhaminiwa na wapiga kura waliosajiliwa wasiopungua mia mbili ambao ni wanachama wa chama chake kutoka kila Mkoa kati ya Mikoa mitano ya Zanzibar;

(b) Uchaguzi wa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi iwapo atadhaminiwa na wapiga kura waliosajiliwa wasiopungua ishirini na tano ambao ni wanachama wa chama chake katika jimbo; au

(c) Uchaguzi wa Diwani iwapo atadhaminiwa na wapiga kura waliosajiliwa wasiopungua kumi na tano ambao ni wanachama wa chama chake katika Wadi.

Dhamana.

**49.**-(1) Kila mgombea, wakati wa kurejesha fomu yake ya uteuzi ataweka kwa Tume au Msimamizi wa Uchaguzi, kwa kadiri itakavyokuwa dhamana ya kiasi cha fedha kilichopangwa na Tume.

(2) Dhamana itakayowekwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itarejeshwa kwa mgombea iwapo atashinda uchaguzi au atapata si chini ya asilimia kumi ya kura halali zilizopigwa au akifariki kabla ya kufungwa upigaji kura.

(3) Dhamana itakayowekwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itachukuliwa na Serikali iwapo mgombea:

(a) atajiondoa katika ugombea baada ya uteuzi;

(b) atapata chini ya asilimia kumi ya kura halali zilizopigwa; au

(c) ameondolewa katika uteuzi.

Uwekaji wazi wa fomu za uteuzi.

**50.** Tume au Msimamizi wa uchaguzi, kwa kadiri itakavyokuwa, mara baada ya muda wa mwisho wa urejeshaji wa fomu za uteuzi uliowekwa na Tume, atazibandika fomu za uteuzi kwa muda wa saa ishirini na nne katika eneo la wazi la ofisi yake.

Pingamizi dhidi ya uhalali wa fomu ya uteuzi.

**51.**-(1) Mgombea anaweza kuweka pingamizi dhidi ya fomu ya uteuzi wa mgombea mwengine kwa moja au zaidi ya sababu zifuatazo; kwamba:

(a) taarifa za mgombea zilizotajwa hazitoshelezi kumtambua mgombea;

(b) ametoa taarifa za uongo katika fomu ya uteuzi; au

(c) fomu ya uteuzi ya mgombea haikuzingatia au haikuwasilishwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(2) Pingamizi yoyote iliyofanywa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itawekwa ndani ya muda rasmi wa uwekaji wazi wa fomu za wagombea.

(3) Mgombea anaweza, kabla ya saa ishirini na nne kabla ya siku ya uteuzi, kuwasilisha pingamizi ya uteuzi kwa:

(a) Tume kwa Uchaguzi wa Rais; au

(b) Msimamizi wa Uchaguzi kwa uchaguzi wa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Udiwani.

(4) Mgombea yeyote ambaye ameweka pingamizi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atawasilisha dhamana katika kiwango kilichoamuliwa na kutangazwa na Tume katika Gazeti.

(5) Dhamana iliyowekwa chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki ,itarejeshwa kwa mgombea iwapo tu mgombea ameshinda pingamizi yake.

(6) Pingamizi iliyowekwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatiwa saini na mgombea na itaeleza sababu za pingamizi katika fomu iliyoandaliwa iliyotayarishwa na Tume.

(7) Tume au Msimamizi wa Uchaguzi anaweza, ndani ya kipindi cha saa ishirini na nne kutoka muda wa mwisho wa uwasilishaji wa pingamizi, kusikiliza kwa uwazi pingamizi iliyowekwa na pande zote zinaweza kuita mashahidi na nyaraka yoyote ambayo inahusiana na pingamizi iliyowekwa.

(8) Tume au Msimamizi wa Uchaguzi anaweza kuamua ipasavyo juu ya uhalali wa kila pingamizi, na atazijulisha pande zote juu ya uamuzi wake.

(9) Pale katika mazingira yoyote, fomu ya uteuzi inapowasilishwa bila ya kuambatanishwa na nyaraka zilizoainishwa katika kanuni itahesabika kuwa ni batili.

Isipokuwa kwamba, Tume au Msimamizi wa Uchaguzi katika mazingira yoyote anayoona inafaa, ataelekeza kuwa fomu hiyo ya uteuzi ikubalike kuwa ni halali hata kama haikuambatanishwa na nyaraka husika na ikiwa nyaraka hizo ziwasilishwe kwa Tume au Msimamizi wa Uchaguzi ndani ya muda mwengine kama ulivyoruhusiwa.

Rufaa dhidi ya Uamuzi wa uteuzi.

**52.**-(1) Mgombea yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi uliofanywa chini ya kifungu cha 51 (8) cha Sheria hii, anaweza kukata rufaa kwa Tume katika kipindi cha saa arobaini na nane tokea uamuzi wa pingamizi kutolewa.

(2) Rufaa, chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itawasilishwa kwa Tume kupitia fomu iliyotayarishwa chini ya Kanuni.

(3) Tume ndani ya saa arobaini na nane baada ya kupokea rufaa, itazisikiliza na kuzitolea uamuzi na kuziarifu pande husika juu ya uamuzi uliotolewa.

(4) Uamuzi wa Tume juu ya rufaa utakuwa wa mwisho na hautohojiwa na Mahkama yoyote.

Uteuzi wa Viti maalum.

**53.**-(1) Kutakuwa na viti maalum vya wanawake katika Baraza la Wawakilishi kwa mujibu masharti ya kifungu cha 67 cha Katiba.

(2) Kutakuwa na asilimia arobaini ya viti maalum vya Madiwani wanawake katika kila Mamlaka za Serikali za Mitaa baada ya Uchaguzi wa Madiwani katika Uchaguzi Mkuu.

(3) Kwa mujibu wa vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki, kabla ya kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu, kila chama cha siasa ambacho kitashiriki katika uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi au Madiwani, kitapendekeza kwa Tume majina ya wanachama wake wenye sifa za kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Viti Maalum vya Wanawake katika Baraza la Wawakilishi au Madiwani.

(4) Waziri anayehusika na Mamlaka za Serikali za Mitaa anaweza kupendekeza kwa Tume majina ya watu mawili kutoka kila Mamlaka za Serikali za Mitaa kuteuliwa kuwa Madiwani.

Utaratibu wa uteuzi.

**54.**-(1) Tume baada ya kupokea majina ya wagombea wa nafasi za viti maalum vya wanawake itatoa fomu za uteuzi.

(2) Mgombea aliyependekezwa na Chama kwa ajili ya uteuzi wa viti maalum vya wanawake atajaza fomu ya uteuzi na kuirejesha kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi kama itakavyoelekezwa na Tume.

(3) Tume itateua siku maalum kwa ajili ya uteuzi wa viti maalum vya wanawake kabla ya siku ya uchaguzi.

(4) Tume itabandika nakala ya fomu ya uteuzi mahala pawazi nje ya ofisi yake.

(5) Mgombea yeyote wa viti maalum vya wanawake anaweza kumuwekea pingamizi mgombea mwengine wa viti maalumu kwa Tume kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 51 cha Sheria hii.

(6) Tume itasikiliza pingamizi na kuzitolea uamuzi.

(7) Tume inaweza kuweka ada maalumu ambayo haitarejeshwa ya uchukuwaji wa fomu ya uteuzi.

Taarifa ya uteuzi.

**55.**-(1) Tume baada ya kuzihakiki sifa za wagombea wanaopendekezwa nafasi ya viti maalum vya wanawake itakijulisha chama kinachohusika iwapo mgombea huyo anazo sifa au amekosa sifa kwa mujibu wa Katiba na Sheria hii.

(2) Chama baada ya kupokea uamuzi wa Tume kitatayarisha orodha ya majina ya wagombea wanawake wa viti maalum kwa mpangilio wa umuhimu na kuiwasilisha kwa Tume kwa kusuburi idadi ya nafasi kitakazozipata kwa mujibu wa asilimia ya viti kitakavyovipata katika Baraza la Wawakilishi au Madiwani katika mamlaka ya Serikali za Mitaa.

(3) Tume mara baada ya matokeo ya Uwakilishi au Udiwani itatangaza majina ya wagombea walioteuliwa kwa mpangilio wa umuhimu kuwa Wawakilishi wa Viti Maalum au Madiwani.

(4) Tume itapeleka orodha ya majina ya wagombea wanawake wa viti maalumu walioteuliwa kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi au Waziri anayehusika na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama itakayokuwa na kuyachapisha katika Gazeti.

Nafasi ya wazi ya viti maalum vya Wanawake.

**56.**-(1) Spika au Waziri anayehusika na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, mara baada ya kuthibitisha kuwa kuna nafasi ya wazi ya Mjumbe wa Viti Maalum katika Baraza la Wawakilishi au Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutokana na sababu yoyote za kisheria, atamjuulisha Mwenyekiti.

(2) Mwenyekiti baada ya kupata taarifa ya Spika au Waziri anayehusika na Mamlaka ya Serikali za Mitaa juu ya nafasi ya wazi ya viti Maalum vya Wanawake katika Baraza la Wawakilishi au Mamlaka ya Serikali za Mitaa, atakitaka chama ambacho nafasi ya mjumbe wake wa viti maalum iko wazi kuwasilisha jina la mgombea wa kujaza nafasi hiyo.

(3) Tume baada ya kupokea jina la Mgombea wa nafasi ya viti maalumu vya Wanawake, itateuwa jina la mgombea huyo kwa mujibu wa kifungu cha 54 cha Sheria hii.

Taarifa na shahada ya uteuzi.

**57.**-(1)Tume au Msimamizi wa Uchaguzi, kwa kadiri itakavyokuwa, atamuarifu na kumpatia shahada ya uteuzi kila mgombea ambaye hakuwekewa pingamizi au baada ya pingamizi au rufaa ameidhinishwa kugombea.

(2) Tume au Msimamizi wa Uchaguzi anaweza, kwa kadiri itakavyokuwa, katika kutekeleza mamlaka yake ya awali au rufaa, kumuondoa mgombea yeyote.

Mgombea pekee wa Urais.

**58.**-(1) Iwapo kuna mgombea mmoja tu wa Urais ndiye aliyeteuliwa kihalali, Tume itamteuwa mgombea huyo kuwa ni mgombea pekee wa Urais.

(2) Mgombea wa urais aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atakuwa amechaguliwa kuwa Rais iwapo atapata sio chini ya asilimia hamsini na kura moja ya kura halali zilizopigwa.

(3) Iwapo mgombea huyo atashindwa kupata kura zinazohitajika chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Tume itatangaza siku nyengine ya uteuzi.

Mgombea pekee wa Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi au Udiwani.

**59.** Iwapo kuna mgombea mmoja tu wa Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi au Udiwani aliyeteuliwa, Msimamizi wa uchaguzi:

(a) atamtangaza mgombea huyo kuwa ni mgombea pekee; na

(b) atamtangaza mgombea huyo kuwa amechaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Udiwani.

Kujitoa kwa mgombea.

**60.**-(1) Mgombea wa Urais, Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi au Udiwani anaweza kujitoa ugombea wake kwa kuwasilisha taarifa ya maandishi iliyosainiwa na yeye mwenyewe kwa Tume au Msimamizi wa Uchaguzi, kwa kadiri itakavyokuwa, si zaidi ya saa 48 baada ya uteuzi.

(2) Taarifa ya kujiondoa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itaambatanishwa na Hati ya kiapo iliyosainiwa mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu kwa Mgombea wa Urais au Hakimu kwa Mgombea wa Uwakilishi au Udiwani.

Kifo au kukosekana kwa mgombea.

**61.**-(1) Iwapo:

(a) baada ya saa kumi za jioni za siku ya uteuzi hakuna mgombea aliyeteuliwa kihalali; au

(b) wakati wowote baada ya saa kumi za jioni za siku ya uteuzi na kabla ya kutangazwa kwa matokeo, mgombea yeyote wa Urais, Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi au Udiwani amefariki, Tume haraka iwezekanavyo, kupitia tangazo katika Gazeti, itateuwa siku nyengine ya uteuzi isiyopungua siku ishirini na moja.

Isipokuwa kwamba, hakutakuwa na uteuzi mwengine mpya utakaofanyika kwa mgombea yeyote ambaye aliteuliwa kihalali katika uteuzi wa awali, na kila mgombea atahesabika kuwa ameteuliwa, isipokuwa awe ametoa taarifa ya kujiondoa kwake.

(2) Endapo siku nyengine ya uteuzi imewekwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki, Tume itatangaza siku nyengine ya uchaguzi wa Rais, Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi au Udiwani na taratibu zinazohusika zitaanza upya.

## SEHEMU YA TATU
## KAMPENI ZA UCHAGUZI

Kampeni za Uchaguzi.

**62.**-(1) Tume inaweza kutangaza kipindi cha kampeni ambacho hakitapungua siku kumi na tano na hakitazidi siku sitini kutoka siku ya uteuzi.

(2) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mgombea au wakala wake au chama chochote cha siasa kinachogombea katika uchaguzi, kina haki ya kufanya kampeni za uchaguzi kukiwezesha kutangaza sera zake kwa wapiga kura kwa kujadiliwa na kuzingatiwa.

(3) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, kampeni za uchaguzi zitafanyika kwa utaratibu ufuatao:

(a) misafara ya vyombo vya moto, maandamano au mikutano ya hadhara;

(b) vipindi au matangazo ya kisiasa kupitia redio, televisheni na magazeti;

(c) uchapishaji wa mabango, posta au vipeperushi yaliyochapishwa au kurikodiwa katika hali ya kielektroniki; na

(d) shughuli nyengine yoyote kama zitakavyoainishwa katika Kanuni.

(4) Mikutano ya kampeni za uchaguzi itaendeshwa kuanzia saa mbili za asubuhi hadi saa kumi na mbili za jioni katika maeneo yaliyoainishwa katika ratiba ya pamoja ya kampeni.

(5) Kila mtumishi wa umma, Taasisi au mamlaka itawajibika kutoa ushirikiano bila ya upendeleo kwa vyama vya siasa vyote kuviwezesha kuendesha kampeni bila ya vikwazo.

(6) Kipindi cha kampeni chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitamalizika saa ishirini na nne kabla ya kuanza upigaji kura.

Mkutano wa hadhara.

**63.**-(1) Mgombea, wakala au chama cha siasa kinaweza kufanya mkutano au maandamano katika kufanikisha kampeni, iwapo tu:

(a) atawasilisha ratiba yake ya kampeni kwa Tume au Msimamizi wa Uchaguzi; na

(b) atashiriki katika mkutano wa majadiliano wa kupanga ratiba ya pamoja ya kitaifa au ya kiwilaya.

(2) Mgombea, wakala au chama cha siasa kinaweza kufanya mikutano ya hadhara au maandamano kwa mujibu wa ratiba ya pamoja ya kampeni katika maeneo yaliyoainishwa na kukubaliwa wakati wa matayarisho ya ratiba ya pamoja ya kampeni.

(3) Maandamano au mikutano ya hadhara ya kampeni iliyoandaliwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, haitafanywa katika maeneo ya hospitali, taasisi za elimu, majengo ya ibada na maeneo yote yasiyoruhusiwa, Isipokuwa inaweza kufanywa nje ya maeneo haya baada ya muda wa kazi.

(4) Ratiba ya pamoja ya mikutano ya kampeni ya kitaifa na kiwilaya itasambazwa kwa wafuataο:

(a) wagombea na vyama vyao;

(b) Jeshi la Polisi katika ngazi za Taifa, Mkoa na Wilaya; na

(c) Ofisi za Wakuu wa Mikoa wa Wilaya.

(5) Tarehe iliyoainishwa katika ratiba iliyotayarishwa chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, itathibitishwa na mgombea au chama kinachoshiriki kwa maandishi na kuwasilishwa kwa Tume na nakala kwa mamlaka ya Polisi za Wilaya saa ishirini na nne kabla ya kufanyika kwa mkutano wa kampeni.

Vifaa vya kampeni na ubandikaji wake.

**64**.-(1) Tume itatayarisha muongozo wa uchapishaji na ubandikaji wa vifaa vya kampeni ya Uchaguzi katika maeneo ya umma.

(2) Mifano ya vifaa vyote vya kampeni vinavyokusudiwa kutumiwa au kubandikwa, kabla ya kubandikwa au kutumika kwa ajili ya kampeni vitawasilishwa kwa Tume au Msimamizi wa Uchaguzi kwa kupata ridhaa.

(3) Tume au Msimamizi wa Uchaguzi ataruhusu matumizi au ubandikaji wa vifaa vya kampeni ambavyo vimeidhinishwa kabla chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

(4) Chama cha siasa au mgombea atabandika vifaa vya kampeni katika maeneo yanayoruhusiwa baada ya kupata idhini ya mmiliki.

(5) Chama cha siasa au mgombea atahakikisha vifaa vyote vya kampeni chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki,vinaondolewa ndani ya siku thelathini baada ya kutangaza matokeo ya uchaguzi.

Kanuni za Maadili.

**65**.-(1) Tume kwa kushauriana na vyama vya Siasa, Msajili wa Vyama vya Siasa na mamlaka ya Serikali, itatayarisha Kanuni za maadili ya kuongoza shughuli za vyama na wadau wengine katika uchaguzi.

(2) Bila ya kujali kuwepo kwa uhuru wa kujieleza, kupata habari, na kujikusanya kwa mujibu wa Katiba, hakuna mtu wakati wa kampeni atakayetumia lugha za uchochezi, uzushi au matusi au lugha ambazo zitapelekea uvunjifu wa amani ya jamii, uasi, chuki, vurugu au vita.

(3) Chama cha Siasa, mgombea na wafuasi wake atahakikisha vifaa vya kampeni vya wagombea wengine haviharibiwi, havichanwi, havitupwi au kuondolewa.

Kampeni za Vyombo vya habari vya Umma.

**66**.-(1) Wakati wa kipindi cha kampeni, kila mgombea atakuwa na haki ya kurusha hewani ilani ya chama chake kupitia vyombo vya habari vya umma.

(2) Vyombo vya habari vitahakikisha vinasimamia misingi ya usawa, na kutopendelea katika kuhudumia na kutangaza kampeni za uchaguzi kwa kila mgombea na chama chake cha siasa.

(3) Tume kupitia vyombo vya habari vya Umma inaweza kupanga muda sawa wa kutangaza kampeni kwa kila chama cha siasa katika redio, televisheni au gazeti la Serikali ambapo vyama vitaruhusiwa kutangaza kampeni zao.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "ilani ya chama ya Uchaguzi" maana yake ni jambo lolote, maelezo au aina nyengine yoyote ya taarifa inayotolewa moja

kwa moja au vinginevyo katika kuhamasisha kupigiwa kura mgombea au chama cha siasa kinachogombea katika uchaguzi.

(5) Kwa madhumuni ya kukipa nguvu kifungu hiki, Tume kwa maandishi inaweza kutoa miongozo kwa chombo chochote cha habari cha Umma.

## SEHEMU YA NNE
## MATAYARISHO YA UPIGAJI KURA

Maeneo na Vituo vya kupiga Kura.

**67.**-(1) Tume itaanzisha maeneo ya kupigia kura kwa Zanzibar yote na kutakuwa na angalau kituo kimoja cha kupigia kura kwenye kila eneo la kupigia Kura.

(2) Vituo vyote vya kupigia kura vitaanzishwa na kuwekwa katika majengo ya umma ikiwa ni pamoja na skuli, kumbi za kijamii au ofisi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, isipokuwa katika:

(a) kituo cha kijeshi au polisi;

(b) nyumba za kuishi;

(c) jengo la chama cha siasa;

(d) baa au klabu;

(e) jengo la ibada; au

(f) hospitali au kituo cha afya.

(3) Tume, kabla ya siku ya uchaguzi, itachapisha katika Gazeti na kutangaza katika zaidi ya gazeti moja lenye mzunguko mkubwa au kutoa tangazo redioni au kupitia utaratibu mwengine, majina ya maeneo yote ambayo vituo vya kupigia kura vimeanzishwa.

Upangaji wa Vituo vya kupiga Kura.

**68.** Msimamizi wa Uchaguzi, kwa kufuata maelekezo na miongozo ya Tume, atafanya yafuatayo:

(a) atapanga idadi ya kutosha ya vituo vya kupigia kura katika kila eneo la kupigia kura;

(b) atateua kwa kila kituo cha kupigia kura, idadi ya wasimamizi wa kupigia kura watakaojulikana kama wasaidizi wa vituo vya kupigia kura, kama atakavyoona inafaa kumsaidia kwa upigishaji kura;

(c) atamteua kutoka miongoni mwa Wasimamizi wa Kituo cha kupigia kura, mtu ambaye atakuwa ni msimamizi wa kituo atakaejulikana kuwa Msimamizi wa Kituo cha kupigia Kura kwa kusimamia upigaji wa kura na kuhesabu kura;

(d) atateuwa msimamizi wa eneo la kupigia kura na kwa ajili ya kuratibu upigaji na kuhesabu kura katika eneo alilopangiwa;

(e) atakipatia kila kituo cha kupigia kura idadi ya kutosha ya vituturi vya kupigia kura ambavyo kwa maoni yake ni muhimu kumuwezesha kila mpiga kura kuweza kupiga kura yake kwa siri;

(f) ataweka au kusababisha kuwekwa katika sehemu ya wazi nje ya kila kituo cha kupigia kura, mfano wa karatasi ya kura;

(g) atatoa kwa kila kituo cha kupigia kura, matangazo yatakayojumuisha maelekezo kuhusiana na utaratibu wa kupiga kura;

(h) atatoa kwa kila Msimamizi wa kituo, idadi ya vifaa vya upigaji kura kama atakavyohisi ni muhimu na vya kutosha kwa hatua za upigaji kura;

(i) Kwa mujibu wa maelekezo ya Tume, atawapatia wasimamizi wa vituo, nakala za daftari kwa ajili ya vituo vya kupigia kura ambayo ina majina ya wapiga kura wanaoruhusiwa kupiga kura katika kituo hicho; na

(j) Kufanya kazi nyengine kama atakavyoelekezwa na Tume.

Wajibu wa Msimamizi wa kituo.

**69.** Msimamizi wa Kituo aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 68(c) cha Sheria hii, katika kutekeleza kazi zake katika kituo cha kupigia au kuhesabu kura atahakikisha kwamba:

(a) Kituo cha kupigia au kuhesabu kura kimewekwa katika utaratibu mzuri;

(b) kuna vifaa vya kutosha vya kupigia au kuhesabu kura;

(c) kuna mazingira mazuri na ya amani ya kuwawezesha wapiga kura kupiga kura zao;

(d) upigaji au kuhesabu kura unafanyika kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Tume;

(e) wapiga kura waliojiandikisha katika kituo hicho tu ndio wanaopiga kura;

(f) kura zilizopigwa katika kituo zinahesabiwa kwa usahihi na kwa mujibu wa Sheria;

(g) fomu za kupigia, kuhesabu kura na matokeo zinajazwa vizuri na kwa usahihi;

(h) matokeo ya kituo cha kupigia kura yanabandikwa au kuwekwa nje ya kituo cha kupigia kura baada ya kuhesabiwa;

(i) fomu za matokeo za kituo na vifaa vya uchaguzi vinakabidhiwa kwa Msimamizi mara baada ya kukamilika kwa zoezi la kuhesabu kura; na

(j) kwa msaada na ushirikiano wa wakala wa kupigia kura, atatatua au kuamua vyenginevyo kwa kila lalamiko litakalojitokeza katika kituo chake cha kupigia kura au litakalowasilishwa na mgombea, wakala, mpiga kura au mtu mwingine aliyeandikishwa au mwenye haki ya kupiga kura katika kituo cha kupigia kura kinachohusika.

Uwezo wa msimamizi wa kituo.

**70.** Msimamizi wa kituo, katika utekelezaji wa majukumu yake katika kituo cha kupigia kura au kuhesabu kura, atakuwa na uwezo wa:

(a) kumuamuru polisi au afisa wa usalama kuhakikisha sheria na maagizo yanafuatwa;

(b) kumuamuru mtu yeyote kuondoka kituoni iwapo ataridhika kuwa uwepo wa mtu huyo katika kituo cha kupigia kura unahatarisha amani ya kituo hicho;

(c) kumkataza mpiga kura au mtu mwengine yeyote kuingia kituoni na kifaa, zana au chombo kisichoruhusiwa; na

(d) kukataza matumizi ya vifaa vya kielectroniki katika kituo cha kupigia na kuhesabia kura isipokuwa kwa watu walioruhusiwa kwa mujibu wa Kanuni.

Vifaa vya kupigia kura.

**71.**-(1) Tume, kwa madhumuni ya uchaguzi, itapanga na kununua vifaa vya kupigia na kuhesabu kura vya kutosha na vyenye ubora.

(2) Vifaa vya uchaguzi kwa mujibu wa kifungu kidogo ya (1) cha kifungu hiki, vitajumuisha vifaa vifuatavyo:

(a) nakala ya daftari la wapiga kura iliyothibitishwa;

(b) karatasi za kura;

(c) masanduku ya kura;

(d) bahasha;

(e) wino usiofutika;

(f) fomu za kupigia, kuhesabu kura na za matokeo;

(g) kitabu cha kumbukumbu;

(h) taa;

(i) chombo cha kuhifadhia vifaa vya kupigia kura;

(j) mihuri;

(k) vifaa muhimu kwa ajili ya kupigia na kuhesabu kura; na

(l) kituturi na kifaa chengine chochote ambacho Tume itahisi ni muhimu.

(3) Msimamizi wa Uchaguzi kwa mujibu wa miongozo ya Tume, atawajibika kuandaa na kuhakikisha mazingira yote muhimu ya usimamizi, utunzaji, usalama na muhimu kwa ajili ya ulinzi na ubora wa vifaa vyote ikiwa ni pamoja na vifaa nyeti vya kupigia kura.

(4) Msimamizi wa Uchaguzi, kwa mujibu wa miongozo ya Tume, atasambaza vifaa vya uchaguzi kwa Wasimamizi wa Vituo kabla ya upigaji kura na kuvikusanya mara baada ya uchaguzi.

Karatasi ya kura.

**72.**-(1) Tume itatayarisha na kupanga uchapishaji wa karatasi za kura za kutosha zenye utambuzi wa kipekee kwa Urais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

(2) Kila karatasi ya kura itakuwa:

(a) na jina kamili, anuani, kazi, nembo ya chama cha siasa cha mgombea kama inavyoonekana katika fomu ya uteuzi na picha ya mgombea;

(b) yenye uwezo wa kukunjwa na kukunjuliwa;

(c) yenye nambari za uchapishaji zilizofuatana juu yake; na

(d) imeunganishwa na kishina chenye nambari sawa na iliyochapishwa katika karatasi ya kura.

(3) Tume inaweza kuionesha kwa umma karatasi ya kura ya mfano kabla ya uchaguzi.

Sanduku la kupigia kura.

**73.**-(1) Tume itanunua masanduku ya kupigia kura kwa matumizi ya kupigia kura.

(2) Kila sanduku la kupigia kura litatayarishwa katika namna ambayo mpiga kura ataweza kuingiza kura na hataweza kuitoa mara baaada ya kuiingiza.

(3) Sanduku la kupigia kura chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, litakuwa linaonesha kilichomo ndani.

Kituturi.

**74.**-(1) Tume itaweka kituturi kimoja au zaidi ya kimoja katika kila kituo.

(2) Kituturi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitatayarishwa katika utaratibu ambao:

(a) utawezesha mpiga kura kuonekana wakati wa kupiga kura; na

(b) misingi ya kura ya siri inalindwa.

Wakala wa upigaji, kuhesabu na kujumlisha kura

**75.**-(1) Kila chama cha siasa kinaweza kuteua kwa kila kituo cha kupigia kura, kuhesabu kura au kujumlisha kura wakala kwa:

(a) mgombe wa Urais; au

(b) mgombea wa Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi na Udiwani.

(2) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kila chama cha siasa kitaiarifu Tume kwa maandishi kikiainisha majina ya mawakala na vituo au eneo walilopangiwa si zaidi ya siku saba kabla ya siku ya uchaguzi.

(3) Endapo wakala aliyechaguliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, amekuwa hawezi kufanya kazi yake kutokana na sababu yoyote ile, chama cha siasa kinaweza kuteua wakala mwingine kushika nafasi yake na kitamtaarifu kwa maandishi Msimamizi wa Uchaguzi jina na anuwani ya wakala aliyeteuliwa na kituo cha kupigia kura.

(4) Wakala wa upigaji, kuhesabu, na kujumlisha kura kwa kadri itakavyokuwa atakuwa na haki ya:

(a) kuwepo katika eneo au kituo cha kupigia, kuhesabia na majumuisho ya kura, kwa kadiri itakavyokuwa;

(b) kuhakiki taratibu za upigaji, kuhesabu au kujumlisha kura kabla ya kuanza kwake;

(c) kuomba taarifa yoyote kutoka kwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo ambayo anaona ni muhimu zinazohusiana na hatua za upigaji, kuhesabu au kujumlisha kura;

(d) kushauriwa kuhusu swali lolote linalojitokeza juu ya kupiga, kuhesabu au kujumlisha kura; na

(e) kuwasilisha malalamiko kwa njia ya maandishi kuhusu kuridhika au kutoridhika kwake na hatua za upigaji au kuhesabu kura.

(5) Wakala wa kupigia, kuhesabu na kujumlisha kura kwa kadri itakavyokuwa atakuwa na wajibu na majukumu ya:

(a) kushirikiana na Msimamizi wa Uchaguzi, au Msimamizi wa kituo katika majukumu yanayohusiana na upigaji, kuhesabu au kujumlisha kura;

(b) kujizuia kuingilia isivyohalali na katika nia ovu, majukumu ya Msimamizi wa Uchaguzi, au Msimamizi wa Kituo ili asiharibu mwenendo wa upigaji, kuhesabu au kujumlisha kura;

(c) kufanya kazi zake kwa uangalifu na kwa usahihi katika kusimamia haki zake chini ya sehemu hii;

(d) kugundua na kutoa taarifa za udanganyifu; na

(e) kumuwakilisha na kulinda maslahi ya mgombea wake katika kituo.

Kutokuwepo wakala.

**76.** Endapo katika Sheria hii, jambo au kitu kinahitajika au kimeamriwa kushuhudiwa na wakala wa upigaji, kuhesabu au kujumlisha kura za wagombea, kushindwa kuwepo au kutokuhudhuria kwa wakala yeyote katika muda, mahali na wakati ulioteuliwa kwa kazi hiyo, hakutabatilisha kitendo au jambo lililofanywa na Msimamizi wa Uchaguzi, au Msimamizi wa kituo.

Watu wanaoruhusiwa kuwemo katika kituo cha kupigia kura.

**77.**-(1) Watu wafuatao wanaruhusiwa kuwemo ndani ya kituo cha kupigia kura:

(a) Msimamizi wa Kituo na Wasaidizi wasimamizi wa Vituo;

(b) Mpiga kura au mtu anayemsaidia mpiga kura;

(c) wakala wa upigaji kura;

(d) mgombea;

(e) Afisa wa Polisi au Afisa wa Idara Maalum au Afisa mwengine yeyote wa usalama kwa madhumuni ya kusimamia usalama katika zoezi la kupiga kura;

(f) Msimamizi wa Uchaguzi au Msaidizi Msimamizi wa Uchaguzi;

(g) Mjumbe wa Tume au Afisa wa uchaguzi;

(h) Mwangalizi aliyeidhinishwa kwa maandishi na Tume; au

(i) Mtu mwengine yeyote atakayeidhinishwa na Tume.

(2) Watu wafuatao wanaruhusiwa kuwemo ndani ya kituo cha kuhesabu kura:

(a) Msimamizi wa Kituo na Wasaidizi wasimamizi wa Vituo;

(b) wakala wa kuhesabu kura;

(c) mgombea;

(d) Afisa wa Polisi au Afisa wa Idara Maalum au Afisa mwengine yeyote wa usalama kwa madhumuni ya kusimamia usalama katika zoezi la kuhesabu kura;

(e) Msimamizi wa Uchaguzi au Msaidizi Msimamizi wa Uchaguzi;

(f) Mjumbe wa Tume au Afisa wa uchaguzi;

(g) Mwangalizi aliyeidhinishwa kwa maandishi na Tume; au

(h) Mtu mwengine yeyote aliyeidhinishwa na Tume.

(3) Hakuna mtu mwingine yeyote ukiachilia waliotajwa katika vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki, ataruhusiwa kuwa ndani ya eneo la mita mia mbili la kituo cha kupigia au kuhesabia kura.

## SEHEMU YA TANO
## UPIGAJI KURA

Nyakati za kupiga kura.

**78.**-(1) Upigaji kura kwa ajili ya uchaguzi, utaanza saa moja asubuhi na kumalizika saa kumi jioni au muda mwengine kama itakavyoamuliwa na Tume.

(2) Msimamizi wa kituo anaweza, iwapo upigaji kura katika kituo umechelewa kutokana na sababu yoyote au haukuanza katika muda uliowekwa chini ya kifungu

kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kuongeza muda wa upigaji kura katika kituo hicho kwa wakati ule ambao upigaji kura ulichelewa au kusimamishwa.

(3) Pale ambapo wakati wa kufunga kituo cha kupigia kura umefika kuna baadhi ya wapiga kura ambao hawajapiga kura zao, upigaji kura utaendelea hadi mpiga kura wa mwisho atakapopiga kura yake.

Isipokuwa kwamba, Msimamizi wa kituo atamuamuru Afisa wa polisi wa kituo kusimama nyuma ya mpiga kura wa mwisho aliyekuwepo wakati wa kufungwa kwa upigaji kura.

Haki ya muajiriwa.

**79.**-(1) Bila ya kujali masharti yoyote katika mkataba wa ajira, wapiga kura wanaolipwa katika mkataba wa ajira wakiwemo wanaofanya kazi za kupokezana, watakuwa na haki ya kuruhusiwa muda wa kutosha kuwawezesha kutumia haki yao ya kupiga kura.

(2) Kila muajiri, katika siku ya uchaguzi iliyotangazwa na Tume, atampatia kila muajiriwa aliye chini yake ambaye ameandikishwa kuwa mpiga kura muda wa kutosha kumuwezesha mwajiriwa huyo kutekeleza haki yake ya kupiga kura.

(3) Muajiri hatatowa adhabu yoyote, kwa Muajiriwa wake baada kutumia haki yake ya kupiga kura.

Utaratibu wa Kupiga kura.

**80**. Upigaji kura katika uchaguzi wowote utafanyika katika utaratibu ufuatao:

(a) Kila mpiga kura aliyeandikishwa ambaye ana nia ya kupiga kura atakwenda yeye mwenyewe katika kituo na atatoa kitambulisho chake cha kupigia kura kwa Msimamizi wa Kituo;

(b) Msimamizi wa Kituo mara baada ya kupokea kitambulisho cha mpiga kura:

(i) atakichunguza kitambulisho hicho na kulinganisha na taarifa za mpiga kura zilizomo katika daftari;

(ii) atataja kwa sauti jina na namba ya mpiga kura kama zilivyo katika nakala ya daftari;

(iii) atatia alama jina la mpiga kura katika nakala la dafatari; na

(iv) atamuelekeza mpiga kura kwa Msaidizi Msimamizi wa kituo cha kupigia kura kupatiwa karatasi ya kura.

(c) Msaidizi Msimamizi wa Kituo cha kupigia kura, kama alivyoagizwa na Msimamizi wa kituo, ataipiga muhuri karatasi ya kura na kumpatia mpiga kura.

(d) Mpiga kura mara baada ya kupokea karatasi ya kura:

(i) atakwenda katika kituturi na kupiga kura yake kwa ridhaa yake;

(ii) ataikunja karatasi ya kura kama alivyoelekezwa;

(iii) ataitia katika sanduku la kupigia kura; na

(iv) atapakwa wino katika kidole kabla hajaondoka kituoni.

Kupiga kura kwa kusaidiwa.

**81.** -(1) Msimamizi wa kituo, baada ya kupokea ombi kutoka kwa mpiga kura ambaye hawezi kupiga kura mwenyewe kutokana na ulemavu au kutojua kusoma au kuandika, na atakaporidhika kuwa mtu huyo hawezi kupiga kura bila ya msaada:

(a) atatangaza kwa watu waliomo kituoni kuwa mpiga kura hawezi kupiga kura mwenyewe;

(b) ataweka alama juu ya jina la mpiga kura huyo katika daftari;

(c) atajaza fomu ya tamko la mpiga kura aliyesaidiwa; na

(d) ataongozana na mpiga kura na msaidizi wake kushuhudia upigaji kura unavyofanyika.

(2) Mtu aliyeteuliwa kumsaidia mpiga kura atatakiwa kuipiga kura hiyo kama alivyoelekezwa na mpiga kura anayesaidiwa kwa kushuhudiwa na Msimamizi wa kituo.

(3) Mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ataikunja karatasi ya kura kwa namna ambayo haitoonesha utambulisho wa mgombea aliyechaguliwa na mtu aliyemsaidia.

(4) Mpiga Kura au msaidizi wake, kwa kadiri itakavyokuwa, ataitumbukiza karatasi ya kura katika sanduku la kura na Mpiga Kura huyo atahesabika kuwa ameshapiga kura, kwa madhumuni ya Sheria hii.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, mtu atakuwa na sifa ya kusaidia mpiga kura asiyeweza kupiga kura akiwa ni baba, mama, kaka, dada, mume, mke au mtoto wa kiume au wa kike wa wapiga kura au mtu mwengine yeyote ambaye ameteuliwa na mpiga kura anayehitaji msaada na ameandikishwa kuwa mpiga kura.

Isipokuwa kwamba, Msimamizi wa Kituo atamruhusu mpiga kura kusaidiwa kama ameridhika kwamba mpiga kura hawezi kupiga kura na kwamba mtu anayemsaidia hajamsaidia mpiga kura mwengine.

Kura ya mapema.

**82.**-(1) Tume itaweka utaratibu utakaoruhusu upigaji wa kura wa mapema ambao utafanyika siku moja kabla ya siku ya upigaji kura, au siku nyengine yoyote kama itakavyoamuliwa na Tume.

(2) Upigaji kura wa mapema chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utatumika katika Uchaguzi Mkuu au Uchaguzi Mdogo wa Urais pekee, na utahusisha:

(a) Wapiga kura wanaotekeleza majukumu ya uchaguzi kama Msimamizi wa Uchaguzi, Msaidizi Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Askari Polisi, Mjumbe au Mtendaji wa Tume; na

(b) Mpiga kura ambaye atahusika na kazi za ulinzi na usalama siku ya Kupiga kura.

Malalamiko dhidi ya karatasi ya kura iliyoharibika.

**83.** Msimamizi wa kituo, pale mpiga kura amepiga kura yake kimakosa,kwa namna ambayo haitaweza kuhesabiwa kuwa kura halali na mpiga kura huyo ameomba kupatiwa karatasi nyengine ya kura, iwapo ataridhika na ombi la mpiga kura huyo, atampatia karatasi nyengine ya kupigia kura na atatia alama karatasi iliyoharibika na kishina chake kwa kuweka maandishi kuwa karatasi hii iliyoharibika imefutwa.

Malalamiko kabla, wakati na baada ya upigaji kura.

**84.**-(1) Msimamizi wa kituo, haraka iwezekanavyo kabla, wakati na baada ya upigaji kura, atatoa nafasi kwa wakala wa upigaji kura ikiwa yupo kuwasilisha malalamiko katika fomu iliyoandaliwa juu ya namna upigaji kura ulivyoendeshwa katika kituo.

(2) Msimamizi wa kituo atatatua malalamiko yaliyowasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kwa namna bora inayowezekana.

(3) Baada ya kukamilika kwa upigaji kura, Msimamizi wa Kituo ataanda taarifa ya kituo inayoelezea malalamiko yaliyowasilishwa kabla, wakati na baada ya upigaji kura na hatua zilizochukuliwa kwa kila lalamiko.

Ufungaji wa kituo cha kupiga kura.

**85.**-(1) Msimamizi wa kituo, haraka iwezekanavyo baada ya kukamilika kwa upigaji kura, mbele ya wagombea au wakala wa upigaji kura ikiwa yupo:

(a) atafunga kwa kifungio, kipenyo cha juu cha sanduku la kura;

(b) atatayarisha bahasha tofauti za:

(i) karatasi za kura zisizotumika, zilizoharibika au zilizofutwa kwa pamoja;

(ii) vishina vya karatasi za kura zilizotumika;

(iii) nakala ya daftari iliyowekewa alama; na

(iv) taarifa iliyotayarishwa na Msimamizi wa kituo.

(2) Msimamizi wa kituo anaweza kumruhusu mgombea au wakala aliyekuwepo kituoni na ambaye anataka kufunga sanduku kwa kutumia kifungio chake, katika hali ambayo, sanduku halitaweza kufunguliwa.

(3) Msimamizi wa kituo atatangaza kufungwa rasmi kwa kituo cha kupiga kura kwa kujaza fomu zilizowekwa katika Kanuni.

## SEHEMU YA SITA
## KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO

Kuhesabu kura.

**86.**-(1) Msimamizi wa kituo, baada ya kukamilika kwa taratibu za upigaji kura, uliofanyika chini ya kifungu cha 85 cha Sheria hii, atatangaza kituo cha kupigia kura kuwa ni kituo cha kuhesabia kura.

(2) Msimamizi wa kituo kabla ya kuhesabu kura, mbele ya watu walioruhusiwa kuwemo katika kituo cha kuhesabu kura:

(a) atahakikisha idadi ya kura zote zilizopigwa katika kituo;

(b) atahakikisha na kunakili idadi ya wapiga kura waliopiga kura katika kituo;

(c) atahakikisha idadi ya karatasi za kura ambazo hazikutumika;

(d) atahakikisha idadi ya karatasi za kura zilizoharibika;

(e) atahakikisha kuwa kuna uwiano kati ya karatasi za kura zilizotolewa, idadi ya wapiga kura waliopiga kura na idadi ya karatasi za kura zilizotumika;

(f) atachunguza, atakagua na atahakikisha masanduku ya kura na ataruhusu mgombea au wakala wa kuhesabu kuchunguza vifungio vya masanduku yote ya kura kujiridhisha kwamba hayakufunguliwa au kuchezewa;

(g) atakata vifungio; na

(h) atafungua sanduku la kura.

(3) Baada ya kufungua sanduku la kura, Msimamizi wa kituo atatoa na kuhesabu kwa sauti kila kura na kunakili kura zote zilizopatikana katika sanduku la kura.

(4) Baada ya kura zote zilizomo katika sanduku kujulikana, Msimamizi wa kituo atazihesabu kura kwa:

(a) kuifungua, kuionyesha na kuiweka katika fungu lake kila kura na kutangaza kwa sauti mgombea ambaye amepata kura hiyo au kama kura hiyo haikuchagua, au vinginevyo sio halali;

(b) kuipanga kila kura katika kundi lake ikiwa imeelekea juu kwa mujibu wa mgombea aliyepata kura hiyo au haikuchagua au vinginevyo sio halali; na

(c) kwa sauti atahesabu na kunakili kura za kila kundi na kuzipatanisha idadi ya kura zote kwa kuzilinganisha zilizotoka katika sanduku na idadi ya wapiga kura waliopiga kura katika kituo cha kupigia kura.

(5) Msimamizi wa kituo wakati wa kuhesabu kura katika kituo cha kuhesabu kura ataanza na kura za Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Udiwani kwa utaratibu wa kufuatana.

Msimamizi wa kituo kuhesabu kura kwa mara ya pili.

**87**.-(1) Msimamizi wa kituo anaweza, iwapo mazingira yanahitaji kuhesabu tena kwa mara ya pili, kuhesabu tena ikiwa:

(a) ameona hakuna uwiano kati ya idadi ya kura zilizohesabiwa ikilinganishwa na idadi ya kura zilizopigwa; au

(b) ameombwa na wakala au mgombea.

(2) Msimamizi wa kituo iwapo ataombwa kuhesabu tena kura na wakala au mgombea atafanya hivyo si zaidi ya mara mbili.

(3) Msimamizi wa kituo baada ya kuhesabu kura kwa mara ya pili kama alivyotakiwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, ataendelea na taratibu za kukamilisha kuhesabu kura kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 88 cha Sheria hii.

Kukamilisha kuhesabu kura.

**88.**-(1) Msimamizi wa kituo, mara moja baada ya kuhesabu kura zote, atatayarisha fomu ya matokeo ya kituo kwa kila uchaguzi kama ilivyowekwa na Tume, ambayo itajumuisha:

(a) Idadi ya kura halali alizopigiwa kila mgombea;

(b) Idadi ya kura halali;

(c) Idadi ya kura zilizoharibika au zilizokataliwa;

(d) Kura zenye mgogoro;

(e) Jumla ya kura zilizopigwa; na

(f) Idadi ya wapiga kura walioandikishwa.

(2) Msimamizi wa kituo, mara baada ya kujaza fomu ya matokeo, atafanya yafuatayo:

(a) atabandika katika eneo la wazi nakala ya fomu ya matokeo ya uchaguzi katika kituo;

(b) atampatia kila wakala wa kuhesabu kura au mgombea nakala ya matokeo;

(c) atazifunga katika bahasha tofauti kura halali, zisizohalali, zilizoharibika, zenye mgogoro na zilizokataliwa;

(d) atatangaza kura alizopigiwa kila mgombea; na

(e) atatangaza kufungwa kwa kituo cha kuhesabia kura.

(3) Fomu ya matokeo itatiwa saini na Msimamizi wa kituo, mgombea au wakala wa kuhesabu kura wa mgombea, na pale ambapo mgombea au wakala huyo atakataa kusaini fomu Msimamizi ataendelea na hatua zilizosalia.

(4) Msimamizi wa kituo ataandaa taarifa ya matokeo ya kila uchaguzi kwa utaratibu wa kujaza fomu iliyoandaliwa na Tume.

(5) Msimamizi wa kituo atakabidhi kwa Msimamizi wa Uchaguzi, masanduku ya kura, ripoti ya awali ya kituo cha kupigia kura na kura yenye mgogoro kama ipo.

(6) Endapo mgombea au wakala wa kuhesabu kura wa mgombea atakataa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, hataruhusiwa kuwasilisha malalamiko yoyote kuhusu utaratibu wa upigaji au kuhesabu kura katika kituo husika.

Malalamiko baada ya kuhesabu kura.

**89.**-(1) Msimamizi wa kituo, baada ya kuhesabu kura atatoa nafasi kwa mgombea au wakala ikiwa yupo kuwasilisha malalamiko katika fomu iliyowekwa kuhusiana na namna kazi ya kuhesabu ilivyofanyika.

(2) Msimamizi wa kituo atatatua malalamiko yaliyowasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kwa namna bora inayowezekana.

(3) Baada ya kukamilika kwa zoezi la kuhesabu kura, Msimamizi wa Kituo ataandaa taarifa ya kituo inayoelezea malalamiko yaliyowasilishwa kabla, wakati na baada ya upigaji kura na hatua zilizochukuliwa kwa kila lalamiko.

Kura halali.

**90.**-(1) Msimamizi wa kituo wakati wa kuhesabu kura, ataamua kura kuwa halali iwapo:

(a) ina muhuri maalum kama ulivyoidhinishwa na Tume;

(b) imewekewa alama ya vema; na

(c) imechagua mgombea mmoja tu.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Tume inaweza kuikubali alama nyengine yoyote ambayo inaonesha nia ya mpiga kura kuwa ni alama halali.

Kura zisizo halali.

**91.**-(1) Msimamizi wa kituo, wakati wa kuhesabu kura, atahesabu kura ifuatayo kuwa imekataliwa, ikiwa:

(a) haina muhuri maalum;

(b) imeandikwa au imetiwa alama ambayo inamtambulisha mpiga kura;

(c) imeandikwa neno lolote au matusi;

(d) imechanwa au kuharibiwa; au

(e) haikuonesha nia ya mpiga kura kwa mgombea halisi aliyemchaguwa.

(2) Msimamizi wa kituo, kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ataandika nyuma ya kura hiyo neno "IMEKATALIWA" na kuweka saini nyuma kwa kura yoyote ambayo sio halali au imekataliwa.

Kura yenye mgogoro.

**92.**-(1) Iwapo Msimamizi wa Kituo ameikataa kura chini ya kifungu cha 91 (2) cha Sheria hii, na uamuzi wake ukapingwa na mgombea au wakala wa kuhesabu kura, ataandika nyuma ya kura hiyo "KUKATALIWA KUMEPINGWA".

(2) Msimamizi wa kituo ataihesabu kura iliyokataliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kuwa ni kura yenye mgogoro na ataiwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi pamoja na ripoti kwa maamuzi.

(3) Msimamizi wa Uchaguzi kabla ya kufanya majumuisho ya kura, ataitolea uamuzi kura yenye mgogoro na uamuzi wake utakuwa wa mwisho na hautojadiliwa.

Msimamizi wa Uchaguzi kufanya majumuisho na kutangaza matokeo.

**93.**-(1) Msimamizi wa Uchaguzi kwa kufuata miongozo ya Tume, atachagua eneo katika Wilaya yake kuwa kituo cha majumuisho kwa ajili ya majumuisho ya kura.

(2) Msimamizi wa Uchaguzi baada ya kupokea taarifa zote, fomu za matokeo na kuamua uhalali wa kura yenye mgogoro na kabla kujumlisha kura, atatangaza kwa sauti matokeo ya kila kituo katika eneo la jimbo au wadi kwa utaratibu wa mfuatano.

(3) Pale ambapo uchaguzi wa Rais, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Diwani unafanyika wakati mmoja, Msimamizi wa Uchaguzi:

(a) atafanya majumuisho ya Urais, Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi na Udiwani kwa kufuatana kama itavyoelekezwa na Tume.

(b) atafanya majumuisho na kuweka matokeo ya vituo vyote vya jimbo kwa kila uchaguzi kwa kuzingatia fomu za matokeo zilizosainiwa; na

(c) atatayarisha fomu ya matokeo ya Jimbo au Wadi kwa kila uchaguzi kama zilivyotayarishwa na Tume ambayo itajumuisha:

(i) idadi ya kura halali alizopigiwa kila mgombea;

(ii) jumla ya kura halali;

(iii) idadi ya kura zilizoharibika au kukataliwa;

(iv) idadi ya kura zilizopigwa; na

(v) idadi ya wapiga kura walioandikishwa.

(4) Fomu za matokeo ya kila jimbo au Wadi kwa kila uchaguzi chini ya kifungu hiki, zitasainiwa na Msimamizi wa Uchaguzi na mgombea au wakala wake na zitabandikwa nje ya kituo cha majumuisho.

(5) Msimamizi wa Uchaguzi, baada ya majumuisho ya kura zote za uchaguzi wa Rais kutoka katika vituo vyote vya jimbo, atayawasilisha kwa Tume pamoja na taarifa zote chini ya ulinzi imara kuzuia upotevu, udanganyifu au uingiliwaji wa namna yoyote, fomu ya matokeo ya jimbo kwa uchaguzi wa Rais kwa jimbo husika pamoja na fomu za matokeo ya vituo.

(6) Baada ya matokeo ya Uchaguzi wa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Diwani kujulikana, kwa kadiri iwezekanavyo, Msimamizi:

(a) atatangaza kura zote zilizopigwa kwa kila mgombea na atamtangaza mara moja, mgombea iliyepata kura nyingi kuwa amechaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Diwani kwa kadri itakavyokuwa;

(b) atatoa cheti cha ushindi kwa mgombea aliyeshinda; na

(c) atawasilisha kwa Tume, matokeo ya uchaguzi pamoja na taarifa zake zote chini ya usimamizi wa ulinzi madhubuti wa kuzuiya upotevu, ubadilishaji au kuingiliwa:

(i) fomu za matokeo ya kila jimbo au wadi, kama itakavyokuwa, pamoja na fomu za matokeo ya kila kituo; na

(ii) vifaa vyote walivyopokea kutoka katika vituo vyote vya kuhesabia kura.

(7) Tume itasababisha kutangazwa matokeo ya uchaguzi chini ya kifungu kidogo cha (6) cha kifungu hiki katika Gazeti.

Watu wanaoruhusiwa kuwemo katika kituo cha majumuisho.

**94.** Watu wafuatao wanaruhusiwa kuwemo ndani ya kituo cha majumuisho ya kura:

(a) Msimamizi wa Uchaguzi;

(b) Mjumbe wa Tume;

(c) Mkurugenzi au Afisa wa Uchaguzi wa Tume;

(d) Mgombea;

(e) Wakala wa majumuisho;

(f) Afisa wa Polisi au mtu mwengine yeyote anayehusika na masuala ya usalama katika kituo cha majumuisho ya kura;

(g) Mwangalizi aliyeidhinishwa kwa maandishi na Tume; au

(h) Mtu mwengine yeyote aliyeidhinishwa na Tume.

Msimamizi wa Uchaguzi kufanya majumuisho ya kura kwa mara ya pili.

**95.**-(1) Msimamizi wa Uchaguzi anaweza, endapo mazingira yanahitaji wakati wa kujumuisha kura, kujumlisha kura kwa mara ya pili kutoka vituo vyote vya kupigia kura vya jimbo au wadi.

(2) Msimamizi wa Uchaguzi ikiwa baada ya kujumlisha kura kwa mara ya pili akijiridhisha kuwa kuna mlingano wa kura baina ya wagombea waliopigiwa kura nyingi za Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi au Udiwani kama ilivyobainika awali, atatoa taarifa kwa Tume ambayo itateuwa na kutangaza katika Gazeti siku nyengine inayofaa ambayo haitazidi siku thelathini baada ya siku ya uchaguzi kwa ajili ya uchaguzi wa marudio.

Majumuisho na kutangazwa matokeo ya kura za Rais.

**96.**-(1) Tume, baada ya kupokea fomu za matokeo ya Uchaguzi wa Rais kutoka majimbo yote, itafanya uhakiki na kujumuisha hesabu za majimbo yote.

(2) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Tume baada ya uhakiki na majumuisho ya kura zote zilizothibitishwa na kila Msimamizi wa Uchaguzi, itatangaza matokeo ya uchaguzi wa Rais.

(3) Tume itamtangaza mshindi wa uchaguzi wa Urais aliyepata kura nyingi halali zilizopigwa.

(4) Iwapo kumbukumbu kutoka jimbo lolote au sehemu yoyote muhimu kwa ajili ya muendelezo wa kukamilisha majumuisho ya kura imekosekana, Mwenyekiti atachukua hatua muhimu ili kurekebisha hali hiyo, na anaweza kuahirisha majumuisho ya kura kwa kipindi kisichozidi saa kumi na mbili.

(5) Matokeo ya uchaguzi wa Rais yatatangazwa ndani ya saa sabini na mbili tokea kufungwa kwa kituo cha mwisho cha kupigia kura, isipokuwa wakati kukiwa na matatizo ya uchaguzi katika baadhi ya vituo, ndani ya saa sabini na mbili baada ya matatizo hayo kutatuliwa.

Uchapishaji wa matokeo na utoaji wa cheti cha ushindi.

**97.** Tume baada ya kutangaza matokeo ya Urais kwa mujibu wa kifungu cha 96 cha Sheria hii, itatoa cheti cha ushindi kwa Rais mteule na itachapisha au itasababisha kuchapishwa matokeo ya uchaguzi wa Rais katika Gazeti.

Uhifadhi wa nyaraka.

**98.**-(1) Msimamizi wa Uchaguzi, mara baada ya uchaguzi, atazikusanya na kuhakikisha anazihifadhi nyaraka na vifaa vyote vya uchaguzi na kuviwasilisha kwa Tume.

(2) Tume itahakikisha uhifadhi mzuri wa vifaa na nyaraka zote zinazohusiana na mwenendo wa uchaguzi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(3) Tume itasababisha nyaraka zote zinazohusiana na kifungu hiki kuharibiwa baada ya kumalizika muda wa siku tisini tokea siku ya uchaguzi isipokuwa kama itakavyoelekezwa vinginevyo kupitia amri ya Mahakama Kuu kutokana na kesi inayohusiana na uchaguzi.

Katazo la kuonesha namna mpiga kura alivyopiga kura.

**99.-**(1) Msimamizi wa kituo, mgombea, wakala wa upigaji kura au mtu mwengine aliye katika kituo cha kupigia kura hatafanya isipokuwa jambo linaloruhusiwa chini ya Sheria hii:

(a) kutaka taarifa yoyote juu ya mgombea ambaye mtu anakusudia kumchagua au amemchagua katika kituo;

(b) kuwasiliana na mtu yeyote kupata taarifa juu ya mtu aliyempigia kura;

(c) kuwasiliana na mtu yeyote juu ya jina au idadi ya wapiga kura ambao wamepiga kura au ambao hawajaomba kupatiwa karatasi za kura au ambao wamepiga kura katika kituo au juu ya alama maalum aliyotumia kuweka muhuri karatasi ya kupigia kura;

(d) kuwasiliana au kutaka kuwasiliana na mtu yeyote baada ya mtu huyo kupokea karatasi ya kura na kabla mtu huyo hajaitia karatasi hiyo katika sanduku la kura, na

(e) kuwasilisha kwa mtu yeyote taarifa kuhusu idadi ya kura alizopata mgombea katika uchaguzi fulani kabla ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi huo.

(2) Mtu anayemsaidia mtu asiyeona au asiyeweza kupiga kura mwenyewe katika kituo cha kupigia kura, kwa mujibu wa Sheria hii, hatafichuwa au kujaribu kufichuwa taarifa za mpiga kura juu ya mgombea anayekusudia kumpigia kura au aliyempiga kura katika kituo.

(3) Mpiga kura ambaye amepiga kura yake katika uchaguzi wowote, hatalazimishwa katika shitaka linalohusiana na matokeo ya uchaguzi kuelezea namna alivyopiga kura.

## SURA YA NNE
## SEHEMU YA KWANZA
## UANGALIZI WA UCHAGUZI

Mualiko kwa waangalizi wa uchaguzi.

**100.-**(1) Tume inaweza, kwa mujibu wa masharti ya Sheria inayohusiana na Ofisi ya Tume ya Uchaguzi, kualika taasisi za ndani zilizosajiliwa na Waangalizi wa Uchaguzi wa Kimataifa kwa madhumuni ya uangalizi wa uchaguzi.

(2) Kila taasisi ya ndani iliyosajiliwa, kabla ya kupatiwa kibali cha uangalizi, itawasilisha kwa Tume nyaraka zifuatazo:

(a) Katiba ya Taasisi;

(b) cheti cha usajili;

(c) muundo wa uongozi unaotambulika; na

(d) uzowefu wake katika masuala wa uangalizi wa uchaguzi usiopungua vipindi vitatu.

(3) Taasisi ya ndani iliyosajiliwa ambayo haitatimiza masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki haitapewa kibali cha uangalizi.

(4) Tume itasimamia utoaji wa vibali na mienendo ya waangalizi, na katika kufanya hivyo, itampangia kila mwangalizi eneo maalum la kufanyia uangalizi chini ya Sheria hii na Sheria inayohusiana na Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

(5) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, taasisi zilizosajiliwa na zisizosajiliwa za kidini hazitaruhusiwa kushiriki katika uangalizi wa uchaguzi.

Mipaka ya uangalizi wa uchaguzi.

**101.** Mipaka ya uangalizi kwa Waangalizi wa uchaguzi itahusisha shughuli zifuatazo:

(a) Kuangalia uadilifu na kazi za Tume na watendaji wake kwa mujibu wa Sheria hii;

(b) Kuangalia uadilifu na uhalali wa maamuzi yanayotolewa na Tume na maafisa wake wakati wa utatuzi wa migogoro;

(c) Kuangalia uandikishaji wa wapiga kura;

(d) Kuangalia mwenendo wa kampeni za uchaguzi;

(e) Kuangalia upigaji wa kura;

(f) Kuangalia mchakato wa kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi; au

(g) Kuangalia fursa ya matumizi ya vyombo vya habari.

Kipindi cha uangalizi.

**102.** Kipindi cha uangalizi wa uchaguzi kitaanza baada ya Mwangalizi kupewa kibali na Tume ambacho kitamalizika muda wake baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi ya kitaifa au baada ya utatuzi wa migogoro yote ya uchaguzi.

Ushirikiano na mamlaka zenye uwezo.

**103.** Tume na mamlaka nyengine za umma Zanzibar, zinaweza kushirikiana na waangalizi wa uchaguzi wakati wa utekelezaji wa majukumu yao na kuwapatia uhakikisho na mambo mengine muhimu kwa ajili ya kukamilisha majukumu yao.

Utambulisho na vibali kwa waangalizi wa uchaguzi.

**104.**-(1) Waangalizi watatambuliwa baada ya Tume kuwapatia vibali na taratibu za uendeshaji na usimamizi wa uchaguzi na kitambulisho.

(2) Kila muangalizi aliyepatiwa kibali chini ya Sheria hii, wakati wa kutekeleza kazi zake atatumia na atavaa kitambulisho cha uangalizi kilichotolewa kwake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

Wajibu wa waangalizi.

**105.**-(1) Waangalizi wa Uchaguzi watakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kuendesha majukumu yao kwa uadilifu, uhuru na malengo;

(b) kuheshimu Sheria za Zanzibar na za Jamhuri ya Muugano wa Tanzania;

(c) kutoingilia au kuzuia shughuli za utendaji wa uchaguzi;

(d) kulinda siri za upigaji wa kura; na

(e) kuipatia Tume nakala ya maandishi na taarifa watakazoziandika na maelezo watakayotoa.

(2) Tume inaweza kufuta kibali cha mwangalizi yeyote ambaye kwa makusudi atashidwa kutekeleza majukumu yake kama yalivyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki na hadhi yake ya uangalizi itaisha.

## SEHEMU YA PILI
## ELIMU YA WAPIGA KURA

Mtaala wa elimu ya mpiga kura.

**106.**-(1) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria inayohusiana na Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Tume inaweza kutayarisha mtaala wa elimu ya wapiga kura utakaotumiwa na wadau wa uchaguzi wanapotoa elimu ya wapiga kura.

(2) Mtaala wa Elimu ya Wapiga kura kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki utahusu elimu ya wapiga kura, taarifa kwa wapiga kura na vipindi vya ushajiishaji wa wapiga kura.

(3) Taasisi yoyote yenye nia ya kuendesha elimu ya wapiga kura mbali na mtaala uliotayarishwa na Tume itawajibika kabla ya kuutumia mtaala huo kuomba ruhusa kwa Tume.

(4) Tume inaweza katika kutumia uwezo wake chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, kukataa sehemu yoyote au maudhui ya Elimu ya Wapiga kura inayotarajiwa kutolewa na taasisi hiyo endapo itafikiria kuwa mtaala wake unakwenda kinyume na mtaala uliotayarishwa na Tume.

Kibali cha kutoa elimu ya wapiga kura.

**107.**-(1) Taasisi yoyote inaweza kuomba kwa Tume kupewa kibali cha kuendesha Elimu ya Wapiga Kura katika awamu yoyote ya mzunguko wa uchaguzi.

(2) Taasisi itakayopewa kibali cha kuendesha elimu ya Wapiga Kura, italazimika kabla ya kuendesha ratiba yake katika Wilaya yoyote, kufanya mashauriano na kushirikiana na Afisa wa Uchaguzi wa Wilaya hiyo.

Kipindi cha kutolewa kwa elimu ya wapiga kura.

**108.** Kwa madhumuni ya Sheria hii, Tume itaandaa au itasababisha kuandaliwa mpango wa elimu ya mpiga kura katika awamu zote za mzunguko wa uchaguzi.

## SURA YA TANO
## UTATUZI WA MIGOGORO NA MALALAMIKO YA UCHAGUZI

Utatuzi wa migogoro ya uchaguzi.

**109.**-(1) Tume, kwa mujibu wa masharti ya Katiba, itakuwa na wajibu wa kutatua migogoro ya uchaguzi, ikiwemo migogoro inayohusu au inayotokezea kutokana na uteuzi wa wagombea isipokuwa ile inayotokana na malalamiko ya uchaguzi.

(2) Mgogoro wa Uchaguzi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki utatolewa uamuzi katika kipindi cha siku saba tangu kutolewa taarifa ya mgogoro huo katika Tume.

(3) Bila ya kujali kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, endapo mgogoro umetokea kwa mujibu kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki unahusiana na uteuzi wa wagombea au uchaguzi, uamuzi wa mgogoro huo unapaswa kutolewa kabla ya tarehe iliyopangwa kufanyika kwa kampeni.

Malalamiko ya uchaguzi.

**110.**-(1) Malalamiko yanayohoji uhalali wa uchaguzi wa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Diwani yataamuliwa na Mahakama Kuu.

(2) Malalamiko chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki yatasikilizwa na kutolewa uamuzi ndani ya miezi kumi na mbili kutoka siku yaliyowasilishwa malalamiko.

Uwasilishaji wa malalamiko ya uchaguzi.

**111.**-(1) Malalamiko ya kuhoji uhalali wa uchaguzi yatafunguliwa ndani ya siku saba tokea kutangazwa kwa mshindi wa uchaguzi na Msimamizi wa Uchaguzi.

(2) Malalamiko yanaweza kuwasilishwa kwa mlalamikiwa binafsi au kwa kutangazwa katika gazeti linalosomwa na watu wengi nchini.

Gharama za dhamana.

**112.**-(1) Mlalamikaji ataweka dhamana kwa ajili ya malipo ya gharama za uwasilishaji wa malalamiko anayowasilisha ambazo zitalipwa kabla ya kusikilizwa kwa malalamiko chini ya Sura hii.

(2) Mtu anayewasilisha malalamiko kupinga uchaguzi atalipa fedha kama ifuatavyo:

(a) shilingi milioni mbili kwa anayewasilisha malalamiko dhidi ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi; au

(b) Shilingi laki tano kwa anayewasilisha malalamiko dhidi ya Diwani.

(3) Endapo mlalamikaji atashindwa kulipa fedha za dhamana kama inavyotakiwa na kifungu hiki wakati wa kuwasilisha malalamiko, Msajili wa Mahkama Kuu hatapanga tarehe ya kusikilizwa kwa malalamiko yoyote ya uchaguzi.

(4) Gharama za kusikilizwa na kuamuliwa kwa maombi chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki zitalipwa kama ambavyo itaelekezwa na Mahakama Kuu, au kama hakuna maelekezo yaliyotolewa, itakuwa ni sehemu ya gharama za juu za malalamiko.

(5) Mahakama Kuu itarudisha dhamana baada ya kusikiliza pande zote na kutowa uamuzi wa malalamiko.

Utaratibu wa Mahkama Kuu inapopokea malalamiko ya uchaguzi.

**113.** Itakapotokea Malalamiko ya Uchaguzi, Mahkama Kuu itayachunguza malalamiko na:

(a) ikiwa itaona kwamba hakuna ushahidi wa kutosha wa kutoa shufaa inayoombwa inaweza kuyakataa malalamiko hayo mara moja; au

(b) kuweka tarehe ya kusikilizwa malalamiko.

Uwezo wa Mahkama Kuu.

**114.**-(1) Mahkama kuu inaweza, wakati wa kutekeleza mamlaka yake kisheria:

(a) kumwita na kumwapisha shahidi kama vile au, iwapo mazingira yatakuwa hivyo kama vile katika kesi za madai zinazoendeshwa na Mahkama Kuu na itatoa adhabu kwa mtu anayetoa ushahidi wa uongo;

(b) kumwita mtu yeyote kusimama kama shahidi ambaye ataonekana na Mahkama Kuu anahusika katika uchaguzi; na

(c) kumhoji shahidi aliyeitwa au mtu yeyote ambaye hakuitwa kama shahidi katika Mahkama, na kuhojiwa na pande zinazohusika na malalamiko na baada ya kuhojiwa shahidi atahojiwa tena kwa mara ya pili au kwa niaba ya Mlalamikaji na anayejibu malalamiko au mmoja kati yao.

(2) Mtu atakayekataa kutii amri ya kuhudhuria Mahakamani atakuwa ametenda kosa la kuidharau Mahkama.

(3) Amri za awali zinazohusiana na malalamiko ya kupinga matokeo ya Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi au Udiwani zitasikilizwa na kutolewa maamuzi na Mahkama Kuu.

Mtu ambaye anaweza kutoa malalamiko ya uchaguzi.

**115.** Malalamiko ya uchaguzi yanaweza kutolewa na mtu yeyote au zaidi ya wafuatao:

(a) mtu ambaye amepiga kura kwa mujibu wa sheria katika uchaguzi huo ambao malalamiko yake yanahusika; au

(b) mtu ambaye ni mgombea katika uchaguzi huo.

Shufaa.

**116.** Mlalamikaji anaweza katika malalamiko yake kuomba zote au moja ya shufaa zifuatazo:

(a) kutolewa tamko kuwa uchaguzi ni batili;

(b) kutolewa tamko kuwa mgombea aliechaguliwa hakuwa halali; au

(c) kutolewa tamko la kuhesabiwa tena kwa kura.

Uwezo wa Jaji Mkuu wa kutunga kanuni.

**117.** Jaji Mkuu anaweza, mara kwa mara kutayarisha Kanuni juu ya uendeshaji wa malalamiko ya uchaguzi chini ya Sheria hii kama atakavyoona inafaa.

## SURA YA SITA
## MAKOSA

Makosa yanayohusiana na uandikishaji.

**118.** Mtu yeyote ambaye kwa ajili ya uandikishaji wa wapiga kura:

(a) ataandikishwa au atawezesha kuandikishwa mtu mwengine kwa kutoa taarifa za uongo;

(b) ataandikishwa katika zaidi ya kituo kimoja cha uandikishaji;

(c) atamuandikisha mtu mwengine akijua kuwa mtu huyo hana sifa za kuandikishwa;

(d) atazuia uandikishwaji wa mtu mwengine akijua kuwa mtu huyo ana sifa za kuandikishwa;

(e) akiwa na mamlaka ya kufanya hivyo, amekataa kufuta uandikishwaji wa mtu akijua kuwa sio sahihi;

(f) atafanya udanganyifu katika Daftari;

(g) atauza, atanunua, au atampatia kitambulisho cha kupigia kura mtu ambaye hahusiki;

(h) kwa nia ya kudanganya, ataharibu au atabadilisha au atarekebisha kitambulisho cha kupigia kura;

(i) atamiliki isivyo halali kitambulisho cha kupigia kura;

(j) kwa kutumia ghasia, vitisho au lengo ovu, kuzuia uandikishaji wa mtu mwengine;

(k) amefutwa kutoka katika Daftari na akatakiwa kukabidhi kitambulisho cha kupigia kura alichopatiwa na Afisa Uandikishaji lakini akakataa;

(l) kwa makusudi akazuia ugunduzi wa walioandikishwa visivyo halali au ukaguzi wa orodha za wapiga kura; au

(m) bila ya ruhusa akafanya, akatayarisha, akachapisha au akamiliki nyaraka au karatasi inayoaminika kuwa ni Daftari la wapiga kura.

atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi milioni tatu na isiyopungua shilingi laki tatu au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopugua miezi mitatu na kisichozidi miezi sita au adhabu zote faini na kifungo.

Makosa yanayohusiana na fomu za uteuzi.

**119.**-(1) Kila mtu ambaye:

(a) ataghushi au kuichana au kuiharibu karatasi yoyote ya uteuzi, au kuwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi fomu yoyote ya uteuzi akijua kuwa imeghushiwa;

(b) akijua kuwa amemdhamini zaidi ya mgombea mmoja wa Urais;

(c) anatumia au anatishia kutumia nguvu zozote au amri za kushawishi au anamlazimisha mtu mwengine kuweka saini au kumzuwia kuweka saini katika fomu yoyote ya uteuzi;

(d) bila ya sababu za msingi atakusanya fomu za uteuzi na asizirejeshe kwa Tume au kwa Msimamizi wa Uchaguzi kama inavyostahiki; au

(e) kwa madhumuni ya kujipatia fomu za uteuzi akiwa mgombea mweyewe au kwa mtu mwengine kwa kujuwa, akatoa maelezo yoyote ya uongo juu ya uteuzi huo katika fomu ya uteuzi, fomu ya maelezo

yake binafsi au hati ya kiapo atakavyoviwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi; au

(f) atatoa maelezo, atachapisha au kutangaza taarifa juu ya kujitoa mgombea yeyote kwa ajili ya kumpendelea mgombea mwengine wa uchaguzi.

atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi milioni tano na isiyopungua shilingi laki tano au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopugua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote faini na kifungo.

Makosa yanayohusiana na Kampeni.

**120.** Mtu yeyote kuhusiana na kampeni za uchaguzi:

(a) ataendesha mkutano wa hadhara kinyume na kifungu cha 62 cha Sheria hii;

(b) atazuia kufanyika, au ataingilia mkutano wa hadhara unaoendelea ulioruhusiwa kwa mujibu wa kifungu cha 62 cha Sheria hii;

(c) atakikatalia chama chochote cha siasa kukipatia huduma sawa kama aliyotoa kwa chama chengine chochote cha siasa;

(d) ataharibu, kubadilisha uhalisia, kuchana au katika hali yoyote ile atasababisha sehemu yake au yote kutotumika, kifaa chochote cha kampeni ambacho kimewekwa katika sehemu iliyoruhusiwa au eneo la wazi au kuweka kitu chengine ambacho kitaficha kifaa cha mwanzo;

(e) atatumia lugha ambayo itachochea uchokozi, uzushi au matusi au ambayo itachochea uvunjifu wa amani, machafuko, uhasama au ghasia; na

(f) ataendesha kampeni za uchaguzi katika sehemu isiyoruhusiwa kama vile maeneo ya Jeshi au Vituo vya Polisi, Taasisi za Umma na maeneo ya kazi wakati wa saa za kazi na kwa taasisi za elimu wakati wa vipindi vya masomo.

atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi milioni tatu na isiyopungua shilingi laki tatu au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miezi sita au adhabu zote faini na kifungo.

Kuingilia au kuzuia mkutano wa kampeni au hadhara unaofanyika kisheria.

**121.** Mtu yeyote ambaye, katika mkutano wa kampeni unaofanyika kwa mujibu wa sheria au mkutano wa hadhara, atafanya au atawashawishi wengine kufanya fujo kwa madhumuni ya kuzuia au kuingilia mkutano wa kampeni au mkutano wa hadhara, atakuwa ni mkosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi milioni tatu na isiyopungua shilingi laki tatu au kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi mwaka mmoja au vyote faini na kifungo.

Kuchapisha, kubandika na kuweka sehemu ya wazi machapisho bila ruhusa ya Tume.

**122.** Mtu yeyote ambaye, atachapisha, atatoa chapisho au atasababisha kuchapishwa au kutolewa chapisho, au atabandika au atasababisha kubandikwa au atasambaza au atasababisha kusambazwa mabango au posta yanayohusiana na uchaguzi au kampeni za uchaguzi bila ya kuwa na:

(a) ruhusa ya Tume au Msimamizi wa Uchaguzi kwa kadiri itakavyofaa;

(b) anuani ya mchapishaji.

atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi milioni tano na isiyopungua shilingi laki tano au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote faini na kifungo.

Makosa yanayohusiana na upigaji na kuhesabu kura.

**123.** Mtu yeyote ambaye, kuhusiana na kupiga na kuhesabiwa kwa kura:

(a) huku akijuwa, atakuwepo katika kituo cha kupigia au kuhesabia kura akiwa hajaruhusiwa kuwepo;

(b) akijua kuwa hana sifa za kupiga kura, akapiga kura katika kituo chochote cha kupigia kura;

(c) kwa udanganyifu akatumia shahada ya kupigia kura ya mtu mwengine ili kutumia haki ya kupiga kura;

(d) kwa makusudi akaruhusu haki ya kupiga kura kutumiwa na mtu mwengine ambaye hana haki hiyo;

(e) akifuatana na mtu asiyejiweza au mwenye ulemavu kwa kumsaidia kupiga kura, kwa udanganyifu na kuvunja uaminifu kupiga kura kinyume na matakwa ya anayemsaidia;

(f) ndani ya kituo cha kupigia kura akaonyesha kura yake au kumlazimisha mtu mwengine kwa kutumia nguvu au udanganyifu kuonyesha kura za wengine;

(g) akiwa katika mzunguko wa mita mia mbili za eneo la kupigia kura, kuainisha nani amempigia kura au atamlazimisha mtu mwengine kuainisha kura aliyopiga mtu mwengine;

(h) kutumia au kutishia kwa kufanya fujo au kutoa taarifa za uongo au njia nyengine za udanganyifu kushawishi kwa nguvu au kumfanya mtu mwengine kupiga kura kumuunga mkono au kumkataa mgombea fulani au mgombea wa chama maalum cha siasa au kutokwenda kupiga kura;

(i) akiwa mtumishi wa umma atatumia ofisi yake kulazimisha au kumshawishi mtu mwengine kupigia kura au kutopigia kura chama cha siasa au mgombea maalum au kutokupiga kura;

(j) moja kwa moja au kwa njia nyengine, atamfukuza au atatishia kumfukuza mtu mwengine katika ajira yoyote au katika kazi nyengine inayompatia kipato au kumzuiya au kutishia kumzuiya mtu mwengine kupata ajira yoyote ile au kazi nyengine yenye kipato au kuendelea kufanya kazi inayompatia kipato au kutumia au kutishia kutumia adhabu yoyote ile kwa mtu mwengine kwa madhumuni ya kumshawishi mtu huyo kupiga kura kwa, au kwa sababu mtu huyo amepiga kura kwa mgombea maalum au kwa mgombea wa chama fulani cha siasa au kwa sababu mtu mwengine huyo amepiga kura kwa au hakupiga kura kwa mgombea maalum au kwa mgombea wa chama fulani cha siasa au kwa sababu mtu mwengine huyo hakupiga kura;

(k) akiwa Msimamizi wa Kituo cha kupigia kura, atashidwa kuonyesha sanduku la kura kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(l) kinyume na sheria ataingiza karatasi za kura, ndani ya sanduku la kura kabla, wakati au baada ya kumalizika upigaji wa kura;

(m) kwa udangayifu atachukua kwa kuhifadhi au kuficha sanduku la kura lenye karatasi za kura zilizokuwa hazijahesabiwa au kuondoa karatasi ya kura iliyokuwa haijahesabiwa;

(n) akiwa mtendaji wa kituo cha kupigia kura, kwa kukusudia akashindwa kutekeleza dhamana zake kwa lengo la kusaidia kutokea uvunjaji wa taratibu za uchaguzi;

(o) akiwa Mtedaji wa kituo cha kupigia kura, bila ya sababu ya msingi akashindwa kupokea malalamiko, au kushughulikia malalamiko kuhusiana na shughuli zinazoendelea katika kituo cha kupigia kura au kufanya uchunguzi na kutaka kusuluhisha lalamiko;

(p) kuingilia kazi za kawaida za kituo cha kupigia au kuhesabia kura;

(q) kukataa kuondoka katika kituo cha kupigia kura baada ya kuamriwa kufanya hivyo na Msimamizi wa Kituo cha kupigia kura;

(r) akiwa askari polisi mwenye dhamana ya ulinzi aliyetakiwa kupanga askari polisi kwa ajili ya kuimarisha usalama katika kituo cha kupigia kura, ameshindwa kufanya hivyo katika muda unaotakiwa bila ya maelezo yoyote;

(s) kuigiza au kughushi au kwa udanganyifu akaharibu karatasi yoyote ya kura au alama rasmi katika karatasi yoyote ya kura;

(t) bila ya mamlaka, akasambaza karatasi za kupigia kura kwa mtu yeyote;

(u) kwa udanganyifu akaingiza ndani ya sanduku lolote la kura karatasi yoyote isiyokuwa karatasi ya kura ambayo ameruhusiwa kisheria kuingiza;

(v) bila ya ruhusa, akatoa kutoka katika kituo chochote cha kupigia kura, karatasi yoyote ya kura au akipatikana anamiliki karatasi yoyote ya kura nje ya kituo cha kupigia kura;

(w) bila ya ruhusa, ataharibu, atachukua, atafungua au kwa njia nyengine ataingiza karatasi zozote za kupigia kura mbali ya zile ambazo zinatumika kwa lengo la uchaguzi;

(x) akiwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo cha kupigia kura akijua au kwa uzembe atashindwa kuweka alama inayokubaliwa katika karatasi ya kura;

(y) atasababisha usumbufu wowote au atashindwa kufuata maagizo yanayotolewa kisheria na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo cha kupigia, kuhesabu au majumuisho ya kura kwa vyovyote itakavyokuwa, katika sehemu yoyote ambapo Daftari limebandikwa kwa ukaguzi au katika kituo cha kupigia kura au mahala ambapo kazi za kuhesabu kura zinafanyika;

(z) katika hali yoyote, kwa udanganyifu ataharibu, atabadilisha, atauficha, atachana, atarekebisha au ataghushi nyaraka yoyote inayohusiana na uchaguzi; na

(aa) ataghushi, kubadilisha, au kwa udanganyifu ataharibu alama yoyote rasmi inayohusiana na uchaguzi.

atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi milioni tano na isiyopungua shilingi laki tano au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopugua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote faini na kifungo.

Kuvaa au kuonyesha alama au nembo katika kituo cha kupigia kura.

**124.** Mtu yeyote ambaye atavaa au ataonyesha kitu chochote ambacho kinaonyesha au kuashiria kukiunga mkono chama au mgombea ndani ya kituo cha kupigia kura, au sehemu yoyote ndani ya eneo linalozunguka kituo cha kupigia kura, atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi milioni mbili na isiyopungua shilingi laki mbili au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopugua miezi mitatu na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote faini na kifungo.

Kuharibu uasilia wa nyaraka.

**125.** Mtu yeyote ambaye, bila ya ruhusa ya kisheria ataharibu kwa kuchana, kuondoa uasilia, au kuondoa nyaraka yoyote iliyowekwa sehemu ya wazi kwa mujibu wa Sheria hii au nyaraka yoyote ambayo imetayarishwa kwa ajili ya ukaguzi kwa mujibu wa maelekezo ya Sheria hii, atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi milioni moja na isiyopungua shilingi laki mbili au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi miwili na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote faini na kifungo.

Kupiga kura zaidi ya mara moja.

**126.**-(1) Mtu yeyote ambaye:

(a) Atapiga kura au atajaribu kupiga kura, au atashawishi au atamtaka mtu mwengine kupiga kura katika kituo chochote cha kupigia kura ikiwa au kwa ufahamu wake anafahamu kuwa mtu huyo tayari amekwisha kupiga kura katika uchaguzi; au

(b) kwa ajili ya kujipatia kura, atatoa karatasi yoyote ya kupigia kura kwa mtu yeyote au yeye mwenyewe au atampatia mtu mwengine kitambulisho chake au anawashawishi au anampatia mtu mwengine ushawishi au kumlazimisha mtu mwengine kumpa mtu wa tatu kitambulisho cha kupigia kura chake yeye mwenyewe au mtu mwengine.

atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi milioni tano na isiyopungua shilingi laki mbili au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote kulipa faini na kifungo.

Utangazaji wa matokeo kinyume na sheria.

**127.**-(1) Ni marufuku kwa mgombea, chama cha siasa, taasisi au mtu mwengine yeyote, kutangaza matokeo ya uchaguzi kwa njia yoyote ya mawasiliano kabla ya kutangazwa rasmi na Tume.

(2) Mgombea, chama cha siasa, taasisi au mtu mwengine yeyote atakayetangaza matokeo ya uchaguzi au kuitaka Tume kutangaza matokeo kabla ya kuisha kwa muda wa kutangaza matokeo uliopangwa, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atapata moja kati ya adhabu zifuatazo:

(a) Ikiwa mgombea, atatumikia kifungo kwa muda usiopungua miaka mitano na faini isiyopungua shilingi milioni hamsini na hatoruhusiwa kugombea katika uchaguzi kwa kipindi cha miaka kumi;

(b) Ikiwa chama cha siasa au taasisi, adhabu isiyopungua shilingi milioni mia moja;

(c) Ikiwa mtu mwengine, atatumikia kifungo kisichopungua miezi thelathini.

(3) Tume au mtu mwengine yeyote atakayeona masharti ya kifungu kidogo cha (1) na (2) vya kifungu hiki yamevunjwa, atatoa taarifa kituo cha polisi ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi ya uvunjifu huo.

Kuzuiya au Kuibughudhi Tume, Mjumbe au Afisa wa Tume.

**128.** Mtu yeyote ambaye:

(a) atambughudhi Mjumbe wa Tume au Afisa aliyeteuliwa chini ya Sheria hii au atashindwa kutii amri halali ya Mkurugenzi au Afisa; au

(b) ataingilia majukumu, mamlaka na uhuru wa Tume kutoa taarifa au kuagiza kutoa taarifa juu ya jambo lolote ambalo lipo chini ya mamlaka ya Tume.

atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni tano au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopugua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote faini na kifungo.

Kuingilia upigaji wa kura au uandikishaji

**129.** Mtu yeyote ambaye ataonyesha dharau au atamshambulia au kwa njia nyengine yoyote atamzuia mpiga kura ambaye yupo ndani ya mzunguko wa mita mia mbili wa eneo la kituo cha kupigia kura, atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi milioni tano na isiyopungua shilingi laki tatu au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote faini na kifungo.

Rushwa.

**130.**-(1) Mtu yeyote ambaye moja kwa moja au kwa njia nyengine, yeye binafsi au kwa niaba ya mtu mwengine kwa madhumuni ya kupata:

(a) uteuzi wake yeye mweyewe au wa mtu mwengine;

(b) kuajiriwa katika Ofisi au sehemu ya ajira akiwa Msimamizi wa Uchaguzi au Mkuu wa Kituo;

(c) karatasi ya kura;

(d) kitambulisho cha kupigia kura;

(e) matokeo ya uchaguzi yasiyohalali; au

(f) vifaa nyeti vya kituo cha kupigia kura.

atatoa au atakubali kutoa au, ataahidi au ataahidi kutoa au ataidhinisha kutolewa, pesa zozote au kitu cha thamani kwa mpiga kura yeyote au kwa mtu mwengine yeyote kwa madhumuni ya kumshawishi mpiga kura kupiga kura au kukataa kupiga kura.

(2) Mtu yeyote ambaye moja kwa moja au kwa njia nyengine, yeye mwenyewe au kwa niaba ya mtu mwengine, atatoa zawadi, mkopo, ahadi ya kufanya manunuzi, au makubaliano kama ilivyoelezwa kwa mtu yeyote kwa madhumuni ya kumshawishi mtu huyo kwa kumpatia au kuidhinisha kupatiwa matokeo ya uchaguzi ya mtu mwengine.

(3) Mpiga kura yeyote ambaye, kabla au wakati wa uchaguzi wowote moja kwa moja au kwa njia nyengine yeye mwenyewe au kwa niaba ya mtu mwengine, atapokea, atakubali kupokea au atakubali kuingia makubaliano ya fedha, zawadi, mkopo au kitu cha thamani, ofisini, sehemu yake ya ajira au kwa mtu mwegine kwa ajili ya kupiga kura au kukubali kupiga kura au kukataa kupiga kura au kukubali kukataa kupiga kura katika uchaguzi wowote.

(4) Mtu yeyote ambaye, baada ya uchaguzi wowote, moja kwa moja au kwa njia nyengine yoyote, yeye mwenyewe au kwa mtu mwengine yeyote kwa niaba yake, atapokea fedha au vitu vya thamani kuhusiana na mtu yeyote kupiga kura au kukataa kupiga kura, au kumshawishi mtu yeyote kupiga kura au kutopiga kura katika uchaguzi wowote.

atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi milioni tano na isiyopungua shilingi laki tano au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote faini na kifungo.

(5) Makosa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki hayahusiani au kumaanisha kuhusisha fedha zozote zilizolipwa au zilizokubalika kulipwa au kuhusiana na matumizi yoyote halali na gharama zinazolipwa kihalali au kuhusiana na uchaguzi wowote.

Matumizi ya nguvu.

**131.** Mtu yeyote ambaye moja kwa moja au kwa njia nyengine, yeye binafsi au kwa kumtumia mtu mwengine yeyote kwa niaba yake, atatumia au atatishia kutumia nguvu, vitisho, ghasia, au atakataa, au atasababisha au atatishia kusababisha, maumivu yoyote ya muda au ya kiroho, kuharibu, kudhuru au kupoteza,dhidi ya mpiga kura yoyote ambaye amepiga kura au ambaye amekataa kupiga kura katika uchaguzi wowote au ambaye, kwa kumteka nyara, matumizi ya nguvu, au njia zozote za uongo, ataweka kikwazo au kuzuia uhuru wa kupiga kura kwa mpiga kura yeyote pia kumpa au kukataa kumpa kura yake katika uchaguzi wowote, atakuwa amefanya kosa la kutumia nguvu na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi milioni tano na isiyopungua shilingi laki tano au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote faini na kifungo.

Makosa yanayohusiana na elimu ya wapiga kura.

**132.** Mtu yeyote au taasisi ambayo itaendesha elimu ya wapiga kura kinyume na maelekezo ya Sheria hii, itakuwa imefanya kosa na ikipatikana na hatia italipa faini isiyozidi shilingi milioni tano na isiyopungua shilingi laki mbili au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miezi sita au adhabu zote faini na kifungo.

## SURA YA SABA
## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA FEDHA

Gharama zitatolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

**133.** Gharama zote zitokanazo na:

(a) maandalizi ya Daftari na utoaji wa vitambulisho vya kupigia kura;

(b) uendeshaji wa uchaguzi;

(c) elimu ya wapiga kura;

(d) mapitio ya mipaka ya majimbo ya uchaguzi; na

(e) gharama nyengine zozote zinazotokana na masuala yanayohusiana na uchaguzi.

zitalipwa katika Mfuko Mkuu wa Huduma za Serikali.

Msamaha wa ushuru wa stempu.

**134.** Hati yoyote iliyowekwa kwa kula kiapo au uthibitisho kwa mujibu wa vifungu vya Sheria hii, haitatozwa ushuru wa stempu kwa kuzingatia sheria yoyote ile inayotumika kwa sasa kuhusiana na ushuru wa stempu.

## SEHEMU YA PILI
## MASHARTI MENGINEYO

Matumizi ya teknolojia .

**135.** Tume inaweza kutumia teknolojia kama inavyoona inafaa katika shughuli za uchaguzi.

Mafunzo.

**136.** Kwa madhumuni ya kuwa na utaratibu mzuri wa kuendesha hatua za uchaguzi, Tume au Msimamizi wa Uchaguzi anaweza, kuendesha mafunzo kwa watendaji wanaohusika na masuala ya uchaguzi.

Malalamiko kwa Tume.

**137.**-(1) Endapo, Mjumbe au Mwakilishi wake amewasilisha malalamiko kwa Tume ya kudai ukiukwaji wa taratibu katika kupiga, kuhesabu au kujumlisha kura na ikiwa hakuridhika na maamuzi katika ngazi ya jimbo, Tume itachunguza na kuamua na endapo itabainika taratibu zimekiukwa, Tume itachukua hatua inayostahiki kusahihisha kasoro hizo na athari iliyojitokeza.

(2) Endapo Tume kufuatia malalamiko yaliyowasilishwa na mgombea au wakala wake imegundua kuwa upigaji au kuhesabu kura katika kituo kimoja au zaidi cha kupigia kura au katika majimbo umetawaliwa na ukiukwaji wa taratibu kutokana na matendo yasiyohalali ya mpiga kura, chama cha siasa, wakala, au mtendaji wa Tume, inaweza kufuta matokeo ya kituo au jimbo hilo.

(3) Iwapo matokeo ya uchaguzi katika kituo au jimbo moja au zaidi yamefutwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Tume itaendesha uchaguzi ndani ya siku thalathini katika kituo au jimbo hilo.

Kusitisha upigaji kura.

**138.**-(1) Msimamizi wa Uchaguzi anaweza, kabla au katika hatua yoyote ya upigaji kura katika siku ya uchaguzi kusitisha upigaji kura iwapo atagundua kuwa upigaji kura katika jimbo hautawezekana kutokana na ukosefu au upungufu wa karatasi za kura.

(2) Iwapo mwenendo wa kituo chochote cha kupigia kura umeingiliwa au umeharibika kutokana na vurugu au machafuko ya wazi au majanga ya kimaumbile, Msimamizi wa kituo anaweza kusitisha upigaji kura hadi siku nyengine na haraka iwezekanavyo atamtaarifu Msimamizi wa Uchaguzi.

(3) Iwapo upigaji kura umesitishwa katika kituo chochote, muda wa upigaji kura wa siku uliositishwa utakuwa sawa na muda wa siku ya mwanzo na marejeo katika Sheria hii juu ya ufungaji wa kituo yatachukuliwa kama yalivyoelekezwa.

Kuakhirisha uchaguzi.

**139.**-(1) Tume inaweza, iwapo yatatokea mazingira yatakayofanya uendeshaji wa uchaguzi usiendelee katika jimbo au wadi, kuakhirisha uchaguzi katika jimbo au wadi hiyo kwa muda ambao inahisi unatosha.

(2) Iwapo tarehe ya kufanyika uchaguzi imeteuliwa na:

(a) kuna kila sababu ya kuamini kuwa uvunjifu wa amani unaweza kutokea iwapo uchaguzi utafanyika katika tarehe hiyo; au

(b) haitawezekana kuendesha uchaguzi kutokana sababu za majanga ya kimaumbile, au dharura nyengine zozote.

Tume inaweza kuakhirisha uchaguzi katika jimbo au wadi husika na itateuwa siku nyengine ya kuendesha uchaguzi ulioakhirishwa.

(3) Iwapo uchaguzi umeakhirishwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, uchaguzi utafanyika katika muda wa mapema unaowezekana kama itakavyoamuliwa na Tume.

(4) Bila ya kujali masharti ya kifungu hiki, Tume inaweza, iwapo itaridhika kuwa matokeo ya uchaguzi hayataathirika kwa upigaji kura wa maeneo yaliyobadilishiwa siku ya upigaji kura, kutangaza matokeo kabla ya uchaguzi ulioakhirishwa kufanyika.

Kiapo cha kutunza siri.

**140.**-(1) Tume itamtaka kila mtendaji wa uchaguzi, mkalimani, wakala au mtu mwengine aliyeruhusiwa kuwepo katika kituo cha upigaji, kuhesabu au majumuisho ya kura, kula kiapo mbele ya Mkuu wa Viapo, kiapo cha kutunza siri kwa mujibu wa sheria zinazoongoza masuala ya viapo.

(2) Mtu atakayekwenda kinyume na kiapo alichoapia, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatumikia kifungo cha miezi kumi na mbili.

Kukosa sifa kutokana na hatia ya rushwa au vitendo viovu.

**141**. Mtu yeyote ambaye atatiwa hatiani kwa vitendo vya rushwa au vitendo viovu na mahakama yenye mamlaka, pamoja na adhabu nyengine yeyote aliyopewa, atakosa sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura au kupiga kura katika kipindi cha miaka mitano tangu tarehe aliyotiwa hatiani chini ya Sheria hii.

Miongozo.

**142.**-(1) Tume inaweza, chini ya masharti ya Sheria hii, kutoa miongozo ya jumla au mahsusi kuhusiana na majukumu ya Msimamizi wa uchaguzi, Afisa Uandikishaji au watu wengine walioajiriwa kwa madhumuni ya Sheria hii.

Isipokuwa kwamba, hakuna miongozo inayopingana na masharti ya Sheria hii au Kanuni.

(2) Mkurugenzi anaweza, kwa mujibu wa maelekezo ya Tume, kuajiri watendaji kama wanavyohitajika kutekeleza majukumu yaliyoainishwa katika Sheria hii.

Uwezo na mamlaka ya jumla ya Tume.

**143.** Tume, katika kutekeleza majukumu yake ya uchaguzi, itakuwa na uwezo, jukumu na mamlaka ya kuamua jambo lolote linalohusiana na uchaguzi ambalo halikuwekewa masharti yake ndani ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote inayohusiana na uchaguzi na uamuzi wake katika jambo hilo utakuwa wa mwisho na hautohojiwa na Mahkama yoyote.

Kanuni, miongozo na taarifa.

**144.** (1) Tume inaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii na bila ya kuathiri masharti ya jumla inaweza kutunga kanuni:

(a) kwa ajili ya kueleza chochote ambacho kipo chini ya masharti ya Sheria hii;

(b) kuweka fomu, nyaraka au viapo kwa madhumuni ya Sheria hii; na

(c) kuweka utaratibu wa uandikishaji na pingamizi katika Daftari.

(2) Maamuzi, miongozo au matangazo yote ambayo Tume ina Mamlaka ya kutoa au kuagiza, yatachukuliwa yamefanywa kihalali iwapo yatatiwa saini na Mwenyekiti au Mkurugenzi.

Kufuta na kubakiza.

**145.-**(1) Sheria ya Uchaguzi Namba 11 ya 1984, imefutwa.

(2) Bila ya kujali Sheria iliyofutwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitu chochote kilichotendwa au hatua zilizochukuliwa chini ya masharti ya Sheria iliyofutwa, zitachukuliwa kuwa zimefanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 13 Disemba, 2017.

..............................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.***